epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumanne Oktoba 29, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581844
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

BAADA YA MAANDAMANO

**Waziri** atinga kijijini kukabili tembo wakorofi



UKURASA 2

**Simbachawene** akerwa na wakuu wa taasisi kufokea watumishi wenzao



UKURASA 3

**Mtuhumiwa** kutishia kwa bastola atiwa mbaroni na polisi



UKURASA 8

# Baba adaiwa mahari baada ya mwanawe kutomzalia mumewe

UKURASA 10

## YALIYOMO

UKURASA WA 22

### TEN HAG ATIMULIWA UNITED, VAN NISTELROOY KUIONGOZA



KLABU ya Manchester United imemfuta kazi kocha, Erik ten Hag, baada ya kuiongoza klabu hiyo kwa muda wa miaka miwili na nusu.

### Askofu Shoo ataja sifa za anayestahili kura Uchaguzi Serikali Mitaa



UKURASA 2



Ng'ombe wa mahari

## Mikoa mitatu tu yanusurika mlipuko kipindupindu nchini

• **Wizara** yaonya wanaorithi nguo za waliofariki dunia kwa Marburg, Mpox... *Endelea ukurasa 5*

**MICHEZO** FADLU: IKIFIKA FEBRUARI SIMBA HAITOKAMATIKA UK.24

**MAONI,** UK.6



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, akizungumza jana na wananchi wa Kijiji cha Mkiwa wilayani Ikungi mkoani Singida, alipofika kusikiliza malalamiko ya wananchi wa kijiji hicho baada ya kufunga barabara kushinikiza serikali iwadhibiti tembo ambao waliharibu nyumba zao Jumamosi baada ya kuvamiwa makazi yao. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Askofu Shoo ataja sifa kiongozi anayefaa Uchaguzi wa S/Mitaa

**Na Elisante John,** SINGIDA

ASKOFU Mkuu mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo, amewataka Watanzania kujitokeza kushiriki ipasavyo katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuwachagua viongozi wanyenyekevu watakaowaletea maendeleo kwenye maeneo yao.

Vilevile, amewataka wananchi kutowabagua wagombea wanawake kwenye uchaguzi kwa kuwa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan umedhihirisha wanawake wana uwezo wa kuongoza nchi.

Dk. Shoo aliyasema hayo juzi wakati wa ibada maalumu ya kuaga watumishi mbalimbali wastaafu wa KKKT Dayosisi ya Kati iliyofanyika mjini hapa.


Alisema katika uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa mwakani, Watanzania wanapaswa kuchagua wanawake na wanaume lakini walio wanyenyekevu, ambao jamii inawaona wana hofu ya Mungu katika utumishi wao wa kuwaletea maendeleo.

"Ndugu zangu, ni dhambi kubwa kudharau mchango wa wanawake katika maendeleo ya jamii, kwa maendeleo ya kanisa. Hivi sasa kuna mfumo dume ambao umejengwa kwamba wanawake hawawezi.

"Na mfumo huu haupo tu kwa jamii na kwenye siasa, bali upo hata kanisani kuwa wanawake hawawezi. Leo ninasimama hapa kuzungumza kwa niaba ya wanawake hawa, tuone mchango wao na tuwe na wazo kwamba 'wanawake wanaweza'," alisema.

Alitaka jamii kuwaunga mkono wanawake katika uongozi ili wazidi kusimamia maendeleo ya kanisa, jamii na miradi inayoanzishwa na serikali.

Kuhusu watumishi walioagwa ambao wamelitumikia kanisa kwa muda mrefu,



Askofu Dk. Shoo alipongeza Dayosisi ya Kati kwa kuliona suala hilo na kutoa rai kwa madhehebu mengine ya dini nchini kuiga mfano huo ili kuwajengea heshima wazee wanaostaafu na familia zao.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema ibada hiyo ni uthibitisho kwamba kanisa hilo linawathamini wazee hao ambao walitumia muda wao mrefu wa maisha kulitumikia kanisa ambalo hivi sasa linaonekana kupiga hatua kubwa ya maendeleo katika nyanja mbalimbali.

"Nina ombi langu hapa leo, tuna uchaguzi hivi karibuni, niwaombe sana ndugu wananchi, wale wote ambao wamejitathmini na wanaona wanazo sifa, basi wasisite kugombea na sisi ndugu zao tutawachagua.

"Kuhusu salamu za Rais, tumeona hapa zilitolewa na Dk. Syprian Hilinti asubuhi, tunayo imani kubwa sana na mama yetu mpendwa anayetuletea maendeleo," alisema Dendego.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

BAADA YA WANANCHI KUANDAMANA...

# Waziri atinga kijijini kukabili tembo wakorofi

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

SIKU chache baada ya wananchi wa kijiji cha Mkiwa, wilayani Ikungi, mkoani Singida kufunga barabara kuu kushinikiza serikali iwadhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana amezuru kijijini huko akiwa na askari 18 watakaoweka kambi kwa mwezi mmoja kuwadhibiti wanyama hao.

Wanakijiji hao walifunga barabara kuu ya Dodoma-Singida kwa saa mbili baada ya tembo kuvamia makazi yao, wakiharibu nyumba zao na kula chakula chao.

Wananchi hao walipendekeza hatua za kuchukuliwa ni pamoja na serikali kuwavuna tembo wakorofi ambao kila mara wamekuwa wakiharibu mashamba, kubomoa nyumba na hata kusababisha vifo.

Balozi Dk. Chana alifika katika kijiji hicho jana akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na kuzungumza na wananchi wa kijiji hicho kueleza hatua za haraka ambazo zitachukuliwa na serikali katika kuwadhibiti tembo hao.

Alisema hatua ya kwanza itakayochukuliwa ni kutambua mapito ya tembo ambayo yamekuwa yanatumiwa tangu enzi, kuongeza askari kwenye vijiji na kuongeza mabomu baridi yatakayotumika kusukuma wanyama hao waharibifu.

Waziri huyo alisema serikali hivi sasa inafanya sensa ya wanyamapori nchi nzima ili kuangalia namna ya kuwadhibiti wasiendelee kuleta madhara kwa wananchi.

Aliongeza kuwa njia nyingi inayoweza kutumika kudhibiti tembo hao ni kulima mazao kama pilipili na ufuta ambayo yanatoa harufu na hivyo inakuwa si rahisi kwa tembo kufika kwenye mashamba na kufanya uharibifu.

"Tutaendelea kutoa elimu kupitia madiwani na wananchi namna ya kukabiliana wanyamapori wakali na waharibifu na ninawahakikishia hapa tumekuja na timu ya askari ambao wataweka kambi hapa wakiwa na vifaa vya kisasa vya kudhibiti tembo," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima, alisema serikali kuu na wananchi wa mkoa watatoa ushirikiano kwa askari wanyamapori 18 watakaoweka kambi katika kijiji cha Mkiwa.

Halima aliagiza wananchi ambao wamepitia mafunzo ya askari wa akiba (mgambo) waorodheshwe kwa kila kijiji kwa ajili ya kupewa mafunzo ya namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu ambayo yatagharamia na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Pia aliwataka wananchi wanapopata changamoto ya tembo, kupiga simu bila malipo kupitia namba 0800110089 ili askari wanyamapori waweze kufika eneo husika na kuchukua hatua.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, alisema tembo wamekuwa wengi sana katika wilaya ya Ikungi ambapo wanatembea kwa makundi ya tembo 30 hadi 40, hivyo kuna umuhimu wa serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi namna ya kukabiliana na tembo.

Mtaturu alitoa ombi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa mizinga ya nyuki ili kusaidia wananchi wanaothiriwa na tembo kwa kuharibiwa mazao ili waweze kuvuna asali kwa ajili ya kupata fedha za kuendeshea maisha na familia zao.

Alisema wizara pia iwe inalipa haraka fidia kwa wananchi walioathiriwa na tembo tofauti na sasa ambapo fidia hizo zimekuwa zinachukua muda mrefu kulipwa.

Awali, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Kanda ya Kati, Herman Nyanda, alisema matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu yameongezeka katika mkoa wa Singida.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Julai mwaka huu, kulikuwa na matukio 162 na halmashauri zinazoongoza kwa matukio ni za wilaya ya Ikungi, Itigi na Manyoni.

Kamishna Msaidizi Nyanda pia alimweleza Waziri wa Maliasili na Utalii kuwa katika kipindi cha kuanzia Januari 2022 hadi Desemba 2023 kulitokea matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu 359 katika mkoa wa Singida.

Alisema changamoto zinazosababisha kutokea kwa matukio hayo ni kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika shoroba za wanyamapori na kutozingatia mipango ya matumizi ya ardhi ambapo vijiji vingi vyenye mipango havizingatii kutenga maeneo ya shoroba za wanyamapori.

Nao wananchi wa kijiji cha Mkiwa walisema serikali ichukue hatua ya kuwavuna tembo wachache wakorofi ambao wamekuwa wanafanya uharibifu kwenye mashamba, kubomoa nyumba na kusababisha vifo.

"Kwenye kila kundi la tembo, wapo wale ambao ni wakorofi. Tunaomba wavunwe maana hatulali, mazao yetu yanaharibiwa kila siku," alilalama Luka Gilayi, mkazi wa kijiji cha Mkiwa.

Jumamosi iliyopita, wananchi wa kijiji cha Mkiwa walifunga barabara kuu ya Dodoma - Singida kwa magogo ya miti kwa zaidi ya saa mbili wakishiniza serikali ichukue hatua za kuwaondoa tembo ambao wamevamia kijiji hicho na kubomoa nyumba na kula vyakula.

Walichukua uamuzi huo baada ya tembo hao kubomoa nyumba nane na kula vyakula hali iliyoleta taharuki kubwa kijijini huko, hata baadhi ya wenyeji kukimbia ovyo.

Singida ni miongoni mwa mikoa ambayo iko katika ikolojia ya Ruaha Rungwa ambayo ni wa pili kwa kuwa na idadi kubwa ya tembo. Zipo shoroba ambazo wanapita kutoka wanyamapori hao kutoka Hifadhi ya Taifa Ruaha, Pori la Akiba Rungwa na Mhesi na kutokezea Hifadhi ya Werembi.

# Simbachawene akerwa wakuu wa taasisi kufokea watumishi wenzao

**Na Lusungu Helela**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameonesha kukerwa na baadhi ya wakurugenzi na wakuu wa taasisi za serikali wenye tabia ya kuwafokea watumishi walio chini yao, wakiamini kufanya hivyo ndio uongozi.

Amesema baadhi yao hudiriki hata kuwatukana watumishi huku akisisitiza jambo hilo ni kosa kubwa na kama kuna kiongozi anataka kuwa na ufanisi, lakini anafikia hatua ya kutukana watumishi, "hafai kabisa" kwa kuwa zipo kanuni, taratibu na sheria za utumishi wa umma za kuchukua kama mambo hayaendi sawa.

Waziri huyo alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na watumishi wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika Kampasi ya Dar es Salaam, akisisitiza kuwa kiongozi makini hahitaji kununa wala kufokafoka, bali kuchukua hatua.

"Kuna watu walikuwa wanasoma kwa bidii zote ili wapate nafasi kwenye utumishi wa umma ili waje wakomeshe watu. Kuna watu kazi yao kubwa ni kuwashughulikia watu na hiyo ndio raha yao," alionya Simbachawene.

Alisema mshahara hata uwe mkubwa kiasi gani kwa watumishi kama mahali hapo pa kazi hapana amani, pana manyanyaso, hakuna kuthaminiwa na kutambuliwa kwa mchango wao, hapawezi kuwa na ufanisi wa kazi. Waziri Simbachawene alikitaka Chuo cha Utumishi wa Umma kisisubiri kuitwa kitoe mafunzo ya kujengeana uwezo mahali pa kazi pamoja na kuhakikisha kinatoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanapoanza kazi ili waweze kutambua haki na wajibu wao.

Alisema kuwa huko kwenye taasisi za serikali kuna shida kubwa ya migogoro ya watumishi isiyoisha ilhali Chuo cha Utumishi kipo.

"Nilitegemea kuona mnafika kwenye taasisi hizo kwa lengo la kutoa mafunzo kwa watumishi ili mambo yaende, lakini hamfanyi hivyo.

"Ninakutana na mashirika makubwa ya nje yananiomba yakatoe mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi katika taasisi fulani za serikali, wanaona mambo hayaendi sawa ilhali ninyi mpo. Hii si sawa, changamkeni, mna fursa nyingi za kubadilisha utumishi wa umma nchini," aliagiza.

Waziri Simbachawene alisema chuo hicho kinapaswa kifanye mafunzo ili kuepuka watumishi wengi kupelekana mahakamani au Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilhali Chuo cha Utumishi kupitia mafunzo ya kujengeana yangetolewa, ingekuwa mwarobaini na hali isingefikia huko.

Awali, Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Mabonesho, aliishukuru Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchango mkubwa wa kutatua tatizo la watumishi katika chuo ambacho kilikuwa kinakabiliwa na uhaba wa watumishi na hivyo kukwamisha kufikia malengo waliyojiwekea.

UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA

# Waandishi wa habari wapewa angalizo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

AMIDI wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) amevitaka vyombo vya habari kutoa taarifa zitakazowajengea uwezo wapigakura ili wafanye uamuzi sahihi.

Dk. Mona Mwakalinga alitoa rai hiyo jana alipofungua mafunzo namna ya kuripoti Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa waandishi wa redio za kijamii nchini.

Alisema vyombo vya habari vinawajibika kuandaa majukwaa ya mijadala kwa wagombea na wapigakura ambayo yatawezesha kujadiliana kwa uwazi masuala yanayohusu uchaguzi kwa kuzingatia mipaka ya uandishi wa habari.

Alisema vyombo vya habari vinawajibika kusimamia uwazi na kuibua masuala ambayo yanaweza kutia doa mchakato wa uchaguzi na hivyo kuhakikisha kunakuwa na uchaguzi huru na wa haki.

"Ukiyatazama majukumu haya kwa undani, ni dhahiri yanahitaji weledi kuyatekeleza, yanahitaji tuwe na maarifa kwenye uelewa wa namna serikali za mitaa zinavyofanya kazi, sheria zinazosimamia uchakataji na utangazaji habari za uchaguzi pamoja na uelewa wa namna ya kiripoti habari hizo," alisema.

Vilevile, Dk. Mona alisema wananchi wengine hususani maeneo ya vijijini hawatapata nafasi za kusikiliza wagombea, wanategemea kufuatilia kampeni na kufanya chaguo sahihi kupitia vyombo vya habari, hivyo ni vyema kuwa makini wakati wa kuripoti taarifa hizo.

Dk. Mona pia alisema ni kazi ya mwandishi wa habari kutoa taarifa kwa usahihi kutokana na wananchi walio wengi kuamini kila kinachotangazwa kwenye vyombo vya habari ndicho chenye ukweli huku waandishi wakiaminiwa kama walimu wa umma.

Meneja wa Mradi wa Ubora wa Maudhui ya Uandishi wa Habari Tanzania, Dk. Zacharia Malima alisema katika kutekeleza mradi huo, wamekuwa wakifanya utafiti na hata kutoa mafunzo kwa wahariri wa vyombo vya habari kuhusiana na ubora wa maudhui ya vyombo vyao. Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwafundisha waandishi namna ya kuandika habari za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa usahihi na kuzingatia misingi ya uandishi.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Nteghenjwa Hosea, alisema kuwa hivi sasa mchakato wa kuchukua fomu unaendelea huku akisisitiza wenye sifa kuendelea kujitokeza kwa siku zilizobaki.

Nteghenjwa alisema mwamko wa kuchukua fomu ni mkubwa kwa kuwa vyama vyote vya siasa vimetoa wagombea katika uchaguzi huo ambao wameanza kuchukua fomu katika maeneo mbalimbali nchini.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

## TANGAZO LA MWISHO WA MATUMIZI YA BARUA ZA TOLEO (LETTER OF OFFER) ZILIZOTOLEWA NA CDA KATIKA JIJI LA DODOMA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote wanaomiliki Ardhi katika Jiji la Dodoma kwa kutumia barua za toleo "letter of offer" zilizotolewa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) kuwa mwisho wa matumizi ya barua hizo ni tarehe 28/12/2024. Hivyo, wananchi wote wanaomiliki Ardhi kwa barua toleo la CDA wanatakiwa ndani ya kipindi cha siku 60 kuanzia tarehe ya tangazo hili kufanya yafuatayo:-

1. Kuwasilisha barua ya toleo, Ofisi ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Divisheni ya Uendelezaji Makao Makuu - Kitengo cha Ardhi kwa ajili ya uhakiki.
2. Baada ya uhakiki, mwananchi atatakiwa kujaza fomu Namba. 19 kwa ajili ya kupatiwa Hati Miliki.
3. Mwananchi kupata Hati Miliki anatakiwa kuwa nyaraka zifuatazo: -
   a. Nakala halisi ya barua ya toleo.
   b. Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya NIDA
   c. Picha 1 (Passport size)
4. Kwa hiyo baada ya tarehe 28/12/2024 Halmashauri ya Jiji la Dodoma pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hawatatambua tena barua za toleo zilizotolewa kwa wananchi wenye Hati Miliki.

**Tangazo hili limetolewa na:-**

**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**





## TANGAZO

access

# ACCESS BANK TANZANIA LIMITED (ZAMANI IKIJULIKANA KAMA AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-24 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,331 | 5,898 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 33,051 | 16,382 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 31,049 | 39,032 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,978 | 2,548 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 195 | 330 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 31,354 | 19,927 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 152,207 | 143,169 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 16,396 | 14,485 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,519 | 1,519 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,685 | 2,630 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **277,765** | **245.920** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 49,747 | 19,049 |
| 18 | Amana za Wateja | 169,474 | 167,823 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,514 | 4,242 |
| 28 | Madeni | 6,517 | 6,423 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **229,252** | **197.536** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **48,513** | **48,384** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 159,426 | 159,426 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 3,233 | 3,233 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (115,175) | (115,183) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 377 | 219 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 652 | 688 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **48,513** | **48,384** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 27,325 | 17,452 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,803 | 6,233 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,353 | 5,253 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 17.47% | 19.67% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.34% | 4.22% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 71.57% | 79.42% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 54.80% | 58.22% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.06% | 83.23% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 17.31% | -0.80% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 12.95% | -22.67% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBER 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-24 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,218 | 10,850 | 29,781 | 31,509 |
| 2 | Gharama za Riba | (3,833) | (4,603) | (10,838) | (14,310) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6.385** | **6,246** | **18,943** | **17,199** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 110 | 500 | 626 | 1,053 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (61) | (956) | (1,675) | (1,256) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **2.120** | **1,908** | **6,199** | **4.700** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 649 | 621 | 3,074 | 1,548 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 650 | 231 | 1,392 | 906 |
| | 6.3 Gawio | 40 | - | 40 | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 781 | 1,056 | 1,693 | 2,246 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(8,343)** | **(8,188)** | **(23,559)** | **(23.786)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (3,333) | (2,919) | (9,157) | (8,479) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,011) | (5,269) | (14,402) | (15.307) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **211** | **(490)** | **535** | **(2,090)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (53) | (59) | (158) | (176) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **158** | **(549)** | **377** | **(2,266)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **158** | **(549)** | **377** | **(2,266)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 175 | 170 | 175 | 170 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.00 | (0.00) | 0.00 | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.32% | -0.69% | 0.27% | -0.95% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.31% | -8.48% | 1.04% | -11.66% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 98.10% | 100.41% | 93.70% | 108.62% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 12.26% | 3.39% | 12.12% | 3.11% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBER 2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-24 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-24 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 211 | 482 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 884 | 1,472 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (9,099) | (12,815) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 32,350 | (1,509) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 7,983 | 3,034 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (728) | 489 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (13,281) | 72,362 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (53) | (53) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **18,266** | **63,462** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | 36 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (828) | (887) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(828)** | **(851)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 94 | (110,833) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | 20,120 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **94** | **(90,713)** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 17,532 | (28,101) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 24,827 | 52,929 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **42,359** | **24,827** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBER 2024

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **139,306** | - | **(133,683)** | - | - | **3,233** | **8,856** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 377 | - | - | - | **377** |
| Hisa za upendeleo | 20,120 | - | - | - | - | - | **20,120** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (652) | 652 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | 19,176 | - | - | - | **19,176** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **159,426** | - | **(114,798)** | **652** | - | **3,233** | **48,513** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | - | **(120,704)** | - | - | **3,018** | **5,268** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (12,979) | - | - | - | **(12,979)** |
| Hisa za upendeleo | 16,352 | - | - | - | - | - | **16,352** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | 215 | **215** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **139,306** | - | **(133,683)** | - | - | **3,233** | **8,856** |

**Kumbuka:** Baada ya kukamilika kwa mchakato wa ununuzi kwa mafanikio, African Banking Corporation Tanzania Limited imebadilisha jina lake na sasa inaitwa Access Bank Tanzania Limited

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 29-Oct-24 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 29-Oct-24 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 29-Oct-24 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 29-Oct-24 |
| 2 | Mkurugenzi | B. Jonker | | 29-Oct-24 |

# Mikoa mitatu tu yanusurika mlipuko kipindupindu nchini

## ● Wizara yaonya wanaorithi nguo za waliofariki dunia kwa Marburg, Mpox

**Na Salome Kitomari**

WIZARA ya Afya imesema inapotokea mgonjwa wa Marburg na homa ya nyani (Mpox) anafariki dunia, familia inapaswa kuteketeza nguo zake badala ya kuzigawana kwa kuwa ni namna ya kusambaza virusi vya ugonjwa huo.

Vilevile, imesema kuwa hadi sasa ugonjwa wa kipindupindu umeipata mikoa yote isipokuwa Njombe, Iringa na Kilimanjaro, hivyo ni muhimu jamii ikachukua tahadhari zote muhimu ikiwamo kutumia maji safi na salama, kunawa mikono mara kwa mara na kutumia vyoo sahihi.

Hayo yalisema jana na Mratibu wa Uelimishaji na Uhamasishaji Jamii Wakati wa Dharura wa Wizara ya Afya, Oscar Kapera, wakati akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jijini Ilala.

"Kuna tishio kubwa la ugonjwa wa kipindupindu ambacho kimeikumba mikoa yote isipokuwa mitatu, pia homa ya nyani (Mpox) na Marburg iko nchi jirani lakini ni lazima kuchukua tahadhari. Tumeweka afua mbalimbali maeneo ya mipakani na tunatoa elimu kwa umma," alisema.

Mratibu huyo alisema inapotokea mgonjwa wa Marburg amefariki dunia, familia zisitekeleze utaratibu uliopo wa kurithi nguo alizokuwa anazitumia kwa kuwa virusi haviteketei kwa joto la kawaida, bali kwa utaratibu maalumu wa joto la zaidi ya nyuzi joto 100 na kemikali nyingine.

"Wapo wanaosema watafua na kupasi nguo alizokuwa anatumia, sisi tunasema ni muhimu kuteketeza vyote ili kuua virusi. Joto la pasi haliwezi kuua virusi hivyo bali kwa joto la zaidi ya nyuzi joto 100 na kemikali," alibainisha.

Alisema ugonjwa huo huambukizwa kwa kugusa majimaji ya mwili wa mgonjwa kama vile damu, mate, matapishi, kinyesi, machozi, kamasi, jasho au mkojo.

Nyingine ni kugusa au kuosha maiti ya mtu aliyefariki dunia akiwa na dalili za ugonjwa wa Marburg, kugusa vyombo, nguo, matandiko au godoro la mtu mwenye maambukizi ya virusi hivyo, kuchangia vitu vyenye ncha kali na mtu mwenye maambukizi ya ugonjwa huo.

Pia kujamiiana na mtu mwenye virusi vya Marburg, mjamzito kumwambukiza mtoto wake akiwa tumboni au mama kumwambukiza mtoto wake wakati wa kunyonyesha.

Alisema maambukizi ya ugonjwa huo yanaweza kutokea pia kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu iwapo mtu atakula au kugusa mzoga au wanyama wenye virusi vya ugonjwa huo kama vile popo, tumbili, nyani au sokwe.

Kapera alibainisha dalili za ugonjwa huo kuwa ni homa, maumivu ya kichwa, misuli, mwili kuishiwa nguvu, vidonda vya koo, vipele vya ngozi, maumivu ya tumbo, kuhara damu, kutapika kunakoweza kuwa damu na kutokwa na damu sehemu za wazi, mfano puani.

Alisema ugonjwa wa Marburg hauna tiba maalumu, chanjo na kwamba mgonjwa hutibiwa kulingana na dalili zitakazoambatana na ugonjwa huo, mfano kutibiwa homa au kuongezwa damu au maji.

Pia alisema uwezekano wa kuishi huongezeka pale mtu anapopata matibabu kwa wakati kutoka kwenye kituo cha huduma za afya.

Mratibu huyo alisema ni muhimu kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara, kuepuka kugusa au kuosha maiti ya mtu aliyefariki dunia akiwa na dalili za ugonjwa wa Marburg, kuepuka kusalimiana kwa kupeana mikono, kukumbatiana au kubusiana na kuepuka kula au kugusa mizoga au wanyama mafano popo, nyani na tumbili.

Kuhusu Mpox, Kapera alisema ugonjwa huo huambukizwa kwa kung'atwa na wanyama, kukwaruzwa na kula nyama mbichi ya wanyamapori.

Alisema mtu anaweza kuambukizwa kwa kugusana moja kwa moja kwa ngozi baina ya mtu mwenye dalili za Mpox, kugusana kupitia kukumbatiana na kujamiiana.

"Kugusa au kutumia nguo, matandiko au vitu vyenye ncha kali ambavyo vilikuwa vinatumiwa na mgonjwa wa Mpox katika maeneo mbalimbali kama nyumbani, kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na kwenye jamii au mama kwenda kwa mtoto," alisema.

Alisema dalili za ugonjwa huo ni vipele maeneo mbalimbali ya mwili na sehemu za siri ambavyo vinaweza kutofautishwa na vipele vingine kwani huambatana na kuvimba kwa mitoki/tezi.

Kapera alisema dalili zingine ni homa, maumivu ya kichwa, vidonda kooni na maumivu ya viungo ya mwili, ikiwamo misuli na mgongo.

Watu wote wako hatarini hasa ambao kinga zao za mwili ziko chini kama watoto, watu wenye wapenzi zaidi ya mmoja na wataalamu wa afya wanaohudumia wagonjwa wa Mpox, hususani wakati wa kuchukua sampuli.

Wengine ni wanaofanya utafiti kuhusiana na virusi vya Mpox bila kuchukua tahadhari.

Kuhusu matibabu, alisema ugonjwa huo una chanjo ambayo ilikuwa inatumika kukinga pepopunda, na kwamba lengo ni kuzuia maambukizi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

"Kwa ujumla ugonjwa huu hauna tiba maalumu ila mtu hutibiwa kulingana na dalilia alizonazo, mfano kama ana homa atapewa dawa za kutulia homa, kama ana maumivu atapewa dawa za kutuliza maumivu," alisema.

Mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Kinga Wizara ya Afya, Dk. Vida Mmbaga, aliwaeleza waandishi wa habari kuwa katika kipindi Januari hadi Oktoba 24 mwaka huu, jumla ya watu 113 wamefariki dunia kwa ugonjwa wa kipindupindu huku 7,190 wakiugua na kutibiwa.

access

ACCESS BANK TANZANIA LIMITED (FORMERLY KNOWN AS AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED)

MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

**AGENCY BANKING FEE**

| | |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Bill payment | Free |

**Withdrawal Fees**

| Transaction tiers | Access Bank Fees | Government Levy | Total Fees |
|---|---|---|---|
| 0-999 | N/A | - | N/A |
| 1,000-1,999 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000-2,999 | 300 | 11 | 311 |
| 3,000-3,999 | 300 | 19 | 319 |
| 4,000-4,999 | 300 | 39 | 339 |
| 5,000-6,999 | 500 | 70 | 570 |
| 7,000-9,999 | 500 | 88 | 588 |
| 10,000-14,999 | 600 | 224 | 824 |
| 15,000-19,999 | 600 | 427 | 1,027 |
| 20,000-29,999 | 600 | 672 | 1,272 |
| 30,000-39,999 | 700 | 770 | 1,470 |
| 40,000-49,999 | 800 | 1,050 | 1,850 |
| 50,000-99,999 | 900 | 1,435 | 2,335 |
| 100,000-199,999 | 1,000 | 1,771 | 2,771 |
| 200,000-299,999 | 1,100 | 2,058 | 3,158 |
| 300,000-399,999 | 1,200 | 2,450 | 3,650 |
| 400,000-499,999 | 1,200 | 2,870 | 4,070 |
| 500,000-599,999 | 2,000 | 3,640 | 5,640 |
| 600,000-699,999 | 2,000 | 4,480 | 6,480 |
| 700,000-799,999 | 2,000 | 4,970 | 6,970 |
| 800,000-899,999 | 2,000 | 5,264 | 7,264 |
| 900,000-1,000,000 | 2,000 | 6,230 | 8,230 |
| 1,000,001-2,000,000 | 2,300 | 6,580 | 8,880 |
| 2,000,001-3,000,000 | 2,500 | 6,580 | 9,080 |
| 3,000,001 na zaidi | N/A | 7,000 | N/A |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Udhalilishaji wagombea mtandaoni udhibitiwe

**KATIKA** toleo letu la jana, tulikuwa na ripoti maalumu kuhusiana na kadhia ya udhalilishaji mtandaoni wagombea wa nafasi za kisiasa nchini, waathirika wakuu wakiwa ni wanawake.

Baadhi ya wanawake waliokumbwa na udhalilishaji huo, wamesema haufanyiki pasi na kujua madhara yake, bali ni mikakati ya makusudi ya baadhi ya watu kudhoofisha ushiriki wao kwa kuwatia woga na kuwakatisha tamaa kujihusisha na siasa.

Wanasiasa hao wametaja madhila wanayopitia katika mitandao ya jamii, hasa wakati wa mchakato wa uchaguzi, yanajumuisha lugha za matusi, wenza wao kutumiwa ujumbe kwamba wake zao wana uhusiano wa kimapenzi na viongozi wa kisiasa na wale wasiokuwa na watoto, kudhalilishwa kwa "kushindwa kuwazalia waume zao".

Ni madhila waliyoyataja yanawafanya wanawake waogope na kuona kuwa siasa zitaacha doa kwao, hivyo kuwa kikwazo kufikia uwakilishi wa 50/50 katika vyombo vya uamuzi.

Wameitaja mitandao ya kijamii kuwa "sumu kwa wanawake kisiasa", wakisisitiza udhalilishaji huo ni miongoni mwa mambo yanayorudisha nyuma mikakati ya kitaifa inayolenga kufikia usawa wa kijinsia katika siasa, takwimu rasmi za kiserikali zikionesha kundi hilo halina uwakilishi mkubwa katika vyombo vya uamuzi.

Ripoti ya iliyokuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ya mwaka 2020, inaonesha wanawake waliochaguliwa kwa nafasi za udiwani walikuwa asilimia 6.58 (260 kati ya 3,953), viti maalumu walikuwa 1,374 katika halmashauri 184 sawa na asilimia 24.59. Kwa jumla, wanawake walikuwa asilimia 29.24 ya madiwani wote nchi nzima.

Ripoti ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2019 pia inaonesha kuwa kati ya nafasi 11,915 za wenyeviti wa vijiji, wanawake walishinda nafasi 246 sawa na asilimia 2.1, huku wanaume wakishika asilimia 97.9 ya nafasi hizo. Kati ya nafasi 4,171 za wenyeviti wa mitaa, wanawake walishinda nafasi 528 sawa na asilimia 12.6.

Vilevile, Taasisi ya Kitaifa ya Kidemokrasia (NDI) inaonesha kuwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, wanawake waliochaguliwa kwa nafasi za ubunge ni asilimia 9.5, wabunge wa viti maalumu ni asilimia 29, hivyo kufanya jumla ya wabunge wanawake kuwa 142 kati ya 393.

Nipashe pia tunatambua kuna utafiti wa mwaka 2021 uliofanywa na Umoja wa Mabunge ya Afrika (APU), ukihusisha wabunge wanawake 224 kutoka nchi 50, ikiwamo Tanzania. Ulibaini asilimia 80 ya waliohojiwa walipitia ukatili wa kisaikolojia, huku asilimia 46 wakikumbana na ukatili wa kijinsia mtandaoni.

Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ya mwaka 2023, inaonesha kuwapo ongezeko kubwa la udhalilishaji kidijitali na ukatili wa kijinsia mtandaoni nchini, wanawake wakiwa walengwa wakuu, kwa asilimia 56.

LHRC ina lingine la ziada; licha ya unyanyasaji huo, wanawake hawatafuti msaada wa kisheria. Takwimu rasmi za kituo hicho zinaonesha asilimia 65 ya wateja waliotembelea kituo kusaka msaada wa kisheria mwaka huo, walikuwa wanaume.


Kudhalilisha wagombea wanawake mtandaoni si tu kunawanyima nafasi ya kushiriki uchaguzi, bali pia kunawaathiri kisaikolojia na hata kijamii, hivyo mamlaka husika zichukue hatua kudhibiti kadhia hii ikizingatiwa hivi sasa nchi iko katika mchakato wa uchaguzi.

Wadhalilishaji wachukuliwe hatua kwa mujibu wa hatua zilizowekwa kisheria ikiwamo Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, inayoelekeza adhabu ya faini, au/na kifungo cha hadi miaka miwili gerezani.

Vilevile, udhalilishaji unaofanywa dhidi ya wagombea wanawake nchini, unakinzana na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia Tanzania ya Mwaka 2000 inayolenga kuweka mazingira wezeshi, kutatua vikwazo dhidi ya wanawake na kuleta haki na usawa ili kundi hilo lishiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika programu na miradi ya maendeleo.

Tanzania pia imeshatia saini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa Mwaka 1979, unaoelekeza kuondoa aina zote za ubaguzi na uonevu kwa wanawake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tufahamu KKK kwa mtoto ndio mwanzo wa kuneemeka kitaalamu

**ELIMU** ya awali kwa mtoto ni ya muhimu, kwani humjengea mtoto msingi mzuri wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK), humjenga na kumwandaa kujiunga na elimu ya msingi.

Mbali na hayo, elimu hiyo humsaidia mtoto kujua kumudu stadi za awali na pia humsaidia kujua stadi mbalimbali za ubunifu na kukuza lugha na kupanua uelewa wake kwa kujua vitu mbalimbali vinavyomzunguka.

Hatua hiyo ni muhimu ikilinganishwa na watoto ambao hawakupata elimu hiyo. Hivyo, wazazi na walezi hawana budi kuhakikisha wanawapeleka shule ili kupata elimu ya awali.

Serikali ilishaweka utaratibu kwa kila shule ya msingi kuwa na madarasa ya elimu ya awali, kwa ajili ya watoto wadogo ili wanapoanza elimu ya msingi wawe tayari wameshapata maarifa hayo.

Wakati huu tunapoelekea mwisho wa mwaka, wataandikishwa watoto wa elimu ya awali na darasa la kwanza, hivyo ni vyema asiwepo mzazi au mlezi mwenye visingizio vya aina yoyote ya kutomwandikisha mtoto.

Karibu miaka 10 sasa elimu inatolewa bure, hivyo hakuna sababu ya kuendelea kukaa na watoto nyumbani kwa kisingizio cha kukosa ada au kumficha mtoto kwa kuwa na ulemavu ama kwa namna yoyote ile.

Ikumbukwe kuwa, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's) hususani katika lengo Namba 4 la Elimu, ni muhimu jamii kusaidiana na serikali kusimamia na kutimiza lengo hilo kwa kishindo.

Lengo hilo linalofikia mwaka 2030, linagusa mambo mengi ikiwamo ubora wa elimu, ikiwa ni kujenga na kuboresha miundombinu ambayo itachangia mazingira bora ya kujifunza kwa watoto kwa wote.

Inaelezwa kuwa katika nchi maskini duniani, watoto na vijana wenye umri wa kwenda shule, hukabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwamo watoto wa kike kutoenda shule, kwa sababu ya kulazimishwa kuolewa.

Bahati nzuri Tanzania imepiga hatua katika safari ya utimizaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, hasa katika lengo hilo, katika upande wa usajili watoto shuleni, hivyo juhudi hizo zisikwamishwe.

Wazazi na walezi wawawezeshe watoto wao kupata elimu ya awali kwa kuwaondolea vikwazo ambavyo kwa namna moja ama nyingine vinaweza kusababisha wasipate elimu, hasa elimu bora.

Serikali ilishaimarisha na kujumuisha elimu ya awali kwenye mfumo rasmi wa elimu na kuagiza kila shule ya msingi kuwa na darasa la elimu ya awali, ili kumpa kila mtoto fursa ya kupata elimu hiyo.

Hivyo, wazazi na walezi ambao hawana uwezo wa kifedha kupeleka watoto wao shule binafsi, hawana budi kuwapeleka katika madarasa ya elimu ya awali ambayo yapo kila shule ya msingi ya serikali.

Kuwapo darasa la elimu ya awali kunasaidia watoto kuanza elimu ya msingi wakiwa tayari wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu, kuliko kuwaacha walivyo na kujikuta wakiwa 'mbumbumbu'.

Mtoto kuhitimu darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika, ni matokeo ya kutoanzishwa elimu ya awali ambayo ni msingi mzuri kwake wa kumfanya apate uelewa mapema kabla kuanza elimu ya msingi.

Wazazi na walezi wakumbuke kuwa, uhaba wa madarasa katika shule za serikali, unasababisha wanafunzi kurundikana katika chumba kimoja cha darasa na kusababisha ufundishaji na ujifunzaji kuwa mgumu.

Kwa mazingira kama hayo, si rahisi mwalimu kumfikia kila mwanafunzi ama wanafunzi wote kumwelewa, hivyo wale ambao watakuwa hawajapitia elimu ya awali wanaweza wasijue kusoma na kuandika hadi wanahitimu darasa la saba.

Katika elimu ya awali, mwalimu unapaswa kumwezesha mtoto kujenga umahiri husika kupitia shughuli zilizobainishwa, mbinu, zana stahiki za kufundishia na kujifunzia na kupima maendeleo ya mtoto hatua kwa hatua.

Hayo ni baadhi ya yaliyomo kwenye mwongozo Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ambayo imeandaa mtaala na muhtasari wa elimu ya awali unaolenga kuwajengea watoto umahiri uliokusudiwa.

Mwongozo huo umegawanyika katika sura nne, sura mbili za mwanzo zinatoa maelezo mafupi kuhusu uchambuzi wa mtaala na ujifunzaji na ufundishaji katika elimu ya awali.

Sura ya tatu inahusu upimaji maendeleo ya mtoto wa elimu ya awali, na nyingine sura inatoa maelezo kuhusu maandalizi ya ufundishaji na namna ya kuwezesha ujenzi wa umahiri ambao mtoto wa elimu ya awali anastahili kuujenga.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA
## Imetolewa chini ya Kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

Amana Bank
*Pamoja, katika njia sahihi*

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024**

| | SHS '000 Robo Mwaka/ Mwaka wa sasa 30 - 09 - 2024 | SHS '000 Robo Mwaka iliopita 30 - 06 - 2024 |
|---|---|---|
| **A. MALI** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 14,396,319 | 11,247,670 |
| 2. Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 27,882,284 | 23,627,763 |
| 3. Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 0 | 0 |
| 4. Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 13,957,394 | 20,041,978 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 278,274 | 11,166 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 31,936,228 | 38,198,792 |
| 10. Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 1,000,479 | 1,000,479 |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 194,034,607 | 188,159,144 |
| 12. Mali Nyingine | 10,522,888 | 6,147,778 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14. Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 9,913,607 | 9,909,501 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **303,922,080** | **298,344,271** |
| | 0 | 0 |
| **B. DHIMA** | 0 | 0 |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| 18. Amana za Wateja | 231,504,226 | 232,377,270 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20. Amana Maalumu | 20,961,851 | 17,408,453 |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 119,399 | 116,679 |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,185,035 | 1,645,244 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 135,126 | 106,807 |
| 27. Dhima Nyingine | 11,440,201 | 11,178,704 |
| 28. Madeni | 6,750,000 | 6,750,000 |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | 273,095,838 | 269,583,157 |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **30,826,242** | **28,761,114** |
| | | |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 45,060,215 | 45,060,215 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (19,468,816) | (19,468,815) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 5,234,843 | 3,169,717 |
| 35. Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 0 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **30,826,242** | **28,761,114** |
| | | - |
| 38.Dhima Zisizo Dhahiri | 17,198,843 | 10,702,090 |
| 39. Mikopo Chechefu | 11,392,611 | 14,282,378 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 9,145,595 | 9,111,448 |
| 41. Mali Nyingine Chechefu | 275,046 | 275,046 |
| | | |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.1% | 9.6% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.2% | 7.3% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 80.5% | 79.0% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 66.9% | 66.1% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 77.7% | 79.3% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 1.1% | 6.9% |
| (vii) Ongezeko la Mali | 1.9% | 6.7% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNE 2024**

| | SHS'000 Robo ya Mwaka sasa | SHS'000 Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | SHS'000 Limbikizo la Mwaka wa sasa | SHS'000 Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | **30 - 09 - 2024** | **30 - 09 - 2023** | **30 - 09 - 2024** | **30 - 09 - 2023** |
| 1. Faida itokanayo na Mikopo | 7,595,073 | 5,938,129 | 21,116,664 | 15,853,777 |
| 2. Gawio la Faida kwa waweka Amana | (359,142) | (440,681) | (1,052,078) | (1,445,728) |
| 3. Mapato Halisi ya Faida (1kutoa 2) | 7,235,931 | 5,497,448 | 20,064,587 | 14,408,049 |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | (396,986) | (2,848,176) | (121,063) | -2,567,692 |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | -409,979 | (413,999) | -2,735,213 | (1,440,057) |
| | | | | |
| **6. Faida isiyotokana na Mikopo:** | **2,069,694** | **1,842,061** | **6,651,107** | **5,677,978** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 345,297 | 386,039 | 1,351,917 | 912,843 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,724,397 | 1,456,022 | 5,299,191 | 4,765,135 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **7. Gharama za uendeshaji:** | (5,831,787) | (5,240,220) | (16,819,329) | (15,853,873) |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,709,738) | (2,404,405) | (8,050,036) | (7,152,245) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (3,122,048) | (2,835,814) | (8,769,293) | (8,701,628) |
| 8. Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | 2,666,875 | (1,162,886) | 7,040,088 | 224,406 |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | (601,748) | (442,972) | (1,805,245) | (1,328,915) |
| **10. Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | 2,065,128 | (1,605,858) | 5,234,843 | (1,104,509) |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **2,065,128** | **(1,605,858)** | **5,234,843** | **(1,104,509)** |
| | | | | |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 336 | 321 | 336 | 321 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 11.6% | -13.6% | 11.6% | -13.6% |
| 15. Idadi ya Matawi | 10 | 10 | 10 | 10 |
| | | | | |
| BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.69% | -2.31% | 1.74% | -0.53% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7% | -6% | 18% | -6% |
| (iii) Uwiano wa Gharama za uendeshaji na Mapato Ghafi | 67% | 67% | 67% | 67% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya yatokanayo na Mikopo na Wastani wa Mali | 3% | 9% | 9% | 9% |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2024**

| | SHS'000 Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30 - 09 - 2024 | SHS'000 Robo Mwaka Uliopita 30 - 06 - 2024 |
|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 2,065,128 | 2,075,219 |
| Marekebisho kwa Ajili ya | - | - |
| - Uchakavu Katika Mali | 1,313,792 | 1,203,413 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Gharama za ukodishaji | 136,771 | 153,861 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (5,909,610) | (6,574,453) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,680,354 | 18,844,724 |
| - Mabadiliko ya kiwango kinachohitajika na banki kuu kisheria | (144,867) | (896,775) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (832,328) | (449,508) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (3,599,975) | (2,207,289) |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| - Kodi Iliyolipwa | (140,000) | (140,000) |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | (4,430,735) | 12,009,192 |
| | - | - |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaj** | - | - |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (226,325) | (324,734) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (36,816) | (107,500) |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Marekebisho katika mali za Kudumu | - | - |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | (263,142) | (432,234) |
| | - | - |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha** | - | - |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (394,967) | (403,823) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | (394,967) | (403,823) |
| | - | - |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | - | - |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (5,088,844) | 11,173,135 |
| | - | - |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu kwa Mwanzo wa Robo ya Mwaka | 79,236,663 | 68,063,528 |
| | - | - |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo ya Mwaka** | **74,147,819** | **79,236,663** |
| | | |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2024**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyo-bakizwa | Ziada ya Kisheria | Mengi-neyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2023 | | | | | | |
| | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 45,060,215 | 0 | (19,468,815) | - | 0 | 25,591,400 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 5,234,843 | 0 | 0 | 5,234,843 |
| Share zilizouzwa | - | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | - | - | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la Robo ya mwaka** | **45,060,215** | 0 | **(14,233,973)** | 0 | 0 | **30,826,242** |
| | 0 | | 0 | 0 | | 0 |
| Mwaka Uliopita 2022 | 0 | | 0 | 0 | | 0 |
| | 0 | | 0 | 0 | | 0 |
| Salio la mwanzo wa Mwaka | 45,060,215 | 0 | (21,067,846) | 1,203,391 | 0 | 25,195,760 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 395,640 | 0 | 0 | 395,640 |
| Share zilizouzwa | - | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 1,203,391 | (1,203,391) | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **45,060,215** | 0 | **(19,468,815)** | - | 0 | **25,591,400** |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Jina na cheo

**Musa Kitoi**
(Naibu Mkurugenzi Mtendaji) — Imesainiwa Oktoba 24, 2023

**CPA Saidi Mbaruku**
(Mkuu wa fedha) — Imesainiwa Oktoba 24, 2023

**CPA Mwinyi Sekro**
(Mkuu wa Ukaguzi) — Imesainiwa Oktoba 24, 2023

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Joseph Gonsalves**
(Mwenyekiti) — Imesainiwa Oktoba 24, 2023

**Salem Balleith**
(Mkurugenzi) — Imesainiwa Oktoba 24, 2023

UWEZESHAJI
*kwa wastaafu*
Kwa Wastaafu Wanaostahiki wa
PSSSF, HAZINA, NSSF & ZSSF
Amana Bank
*Pamoja, katika njia sahihi*



## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi ambao orodha yao ipo hapa chini waliolipia viwanja kwa nyakati tofauti eneo la Kikombo Kitalu "DA" na "N" kupitia benki, ila taarifa zao zinamapungufu ya majina, namba ya kiwanja na kitalu wafike ya Halmashauri iliyopo Manispaa ya zamani sehemu ya **mauzo ya viwanja** kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao.

Muda wa utekelezaji ni kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2024 hadi tarehe 10 Novemba, 2024.

Kushindwa kufanya hivyo, umiliki huo hautatambulika tena.

**ORODHA YA MAJINA YENYE TAARIFA PUNGUFU**

| NA | JINA | MALIPO |
|---|---|---|
| 1. | Christopher Kasung | 10,000.00 |
| 2. | Mbaga Iyombe | 1,000,000.00 |
| 3. | Veisi Maineko | 42,000.00 |
| 4. | George Abel Ngab | 300,000.00 |
| 5. | Ngalawe Hassan Ramadha | 6,931,641.00 |
| 6. | Esther Mpangala | 5,000,000.00 |
| 7. | Victoria Mgala | 400,000.00 |
| 8. | Godfrey K. Msongwe | 9,096,340.00 |
| 9. | Eliaza Mangera Wangwe | 5,148,000.00 |
| 10. | Florence N. Kebwe | 2,515,000.00 |
| 11. | Ali Hussein Habib | 338,300.00 |
| 12. | Joseph Lukumbika | 265,000.00 |
| 13. | Rosina J Delima | 2,249,554.00 |
| 14. | Kelvin Mlambalamba | 1,200,000.00 |
| 15. | Starphod Marwa | 1,000,000.00 |
| 16. | Ally H. Thabit | 3,000,000.00 |
| 17. | Mariam Tawakel | 10,000.00 |
| 18. | Jeremia Baha | 255,000.00 |
| 19. | Shani Mwaruka | 400,000.00 |
| 20. | Ramadhan N Simba | 50,000.00 |
| 21. | Ally Habiba Thabit | 3,000,000.00 |
| 22. | Job Ndalo | 100,000.00 |
| 23. | Giligoli A Ndaro | 100,000.00 |
| 24. | Gloria Reuben Ndaro | 80,000.00 |
| 25. | Magreth W Luma | 10,000.00 |
| 26. | Chedi Ng'enda | 21,729,382.00 |
| 27. | Sospeter N Marco | 2,500,000.00 |
| 28. | Geophrey Mtweve | 1,150,000.00 |
| 29. | Leonary Kimario | 24,000.00 |
| 30. | Lilian Sebastian | 1,625,000.00 |
| 31. | Anna Elisamehe | 400,000.00 |
| 32. | Olais Peter | 300,000.00 |
| 33. | Mussa Deogratius Limb | 4,566,560.00 |
| 34. | Marium | 225,000.00 |
| 35. | Rainer | 4,607,934.00 |
| 36. | George | 100,000.00 |
| 37. | Jafari | 500,000.00 |
| 38. | Dann | 10,000.00 |
| 39. | Victoria | 1,015,000.00 |
| 40. | Jona | 50,000.00 |
| 41. | Alvin | 677,100.00 |
| 423. | Christina | 700,000.00 |
| 43. | Tina | 100,000.00 |
| 44. | Doreen | 300,000.00 |
| 45. | Kelvin | 1,500,000.00 |
| 46. | Innocent | 1,000,000.00 |
| 47. | Mabrouk | 100,000.00 |
| 48. | SHM | 1,000,000.00 |
| 49. | Khadija | 500,000.00 |
| 50. | Jackline | 40,000.00 |
| 51. | Zubeda | 100,000.00 |
| 52. | Kelvin | 250,000.00 |
| 53. | Antony | 180,000.00 |
| 54. | Stanley | 3,500,000.00 |
| 55. | Kelvin | 250,000.00 |
| 56. | | 2,000,000.00 |
| 57 | | 220,000.00 |
| 58. | | 4,447,406.00 |
| 59. | | 2,000,000.00 |
| 60. | | 5,000,000.00 |
| 61. | | 1,566,355.00 |

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**


# Mtuhumiwa kutishia kwa bastola atiwa mbaroni Dar

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi linamshikilia Derick Junior kwa tuhuma za kumjeruhi na kumtishia kwa silaha, Julian Buhuju baada ya video za tukio hilo kusambaa kwenye mitandao ya kijamii jana.

Video hiyo inamwonesha anayedaiwa kuwa ni Derick akimpiga kwa kitako cha bastola Julian baada ya kuwa katika malumbano ya muda mfupi yanayodhaniwa kuwa ni ugomvi wa kugombea mwanamke.

Video hiyo ilimwonyesha Derick akimtaka mwanamke aliyekuwa ameambana na Julian amfuate yeye, lakini mwanamke huyo hakutaka kuambatana naye, hata kumng'ang'ania Julian.

Wakati malumbano kati ya wawili hao yakiendelea, Julian aliingilia ndipo Derick alipomshambulia kwa ngumi na mateke kisha akatoa bastola na kuiandaa kwa ajili ya kudhuru.

Hata hivyo, silaha hiyo haikutoa risasi na baadaye akawa akampiga na kitako cha bastola katika maeneo ya kichwani na mateke.

Aliendelea kumshambulia kwa mateke ya usoni mpaka pale alipoona kuwa ameishiwa nguvu. Wakati hayo yote yanaendelea, mashuhuda walikuwa wamekaa pembeni wakihofia usalama wao, huku wengine wakijaribu kusogea kwa kuvizia.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na Kamanda wa Kanda Maalum ya Polisi, SACP Jumanne Muliro ilieleza kuwa wamemkamata na wanamshikilia Derick Derick Junior (36), mkazi wa Salasala, Kinondoni kwa tuhuma za kujeruhi na kutishia kwa silaha.

Alisema walichukua uamuzi huo baada ya uchunguzi wao kubaini kuwa Oktoba 27 mwaka huu, wakiwa katika ukumbi wa starehe wa Masaki 1235, saa 12.30 asubuhi, mtuhumiwa alimjeruhi Julian Buhuju kwa kumpiga na kitako cha bastola na kumjeruhi sehemu ya jicho na pua.

"Kitendo hicho hakikubaliki na ni kinyume na sheria. Aliyejeruhiwa anaendelea vizuri na matibabu. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka linakamilisha utaratibu wa kisheria ili mhusika afikishwe katika vyombo vingine vya sheria haraka iwezekanavyo," alisema.

Kamanda Muliro alitoa tahadhari kwa wananchi wanaomiliki silaha kufuata taratibu na kanuni zilizoainishwa kwenye vibali vyao vya umiliki wa silaha kwa kuwa jeshi hilo halitasita kumchukulia hatua mtu yeyote anayemiliki silaha, atakayebainika kufanya matendo ambayo ni kinyume cha sheria, kanuni na taratibu hizo.

# Aweso awahakikishia maji wakazi Dar, Pwani

**Na Frank Monyo**



WAZIRI wa Maji, Juma Aweso amewahakikishia wakazi wa Dar es Salaam na Pwani upatikanaji maji safi na salama katika mikoa hiyo kwa kuwa changamoto ya hitilafu ya mtambo wa kuzalisha maji katika Mtambo wa Ruvu Juu imerekebishwa.

Alitoa kauli hiyo jana alipozuru na kukagua mtambo huo kujionea ukarabati uliofanywa na wahandisi wa DAWASA baada ya kutokea kwa hitilafu katika moja ya mitambo kiasi cha kuathiri uzalishaji majisafi na salama.

"Kwa kawaida mtambo wa Ruvu Juu ukiwa katika hali ya ubora wake, unazalisha maji kiasi cha lita milioni 197 kwa siku, lakini baada ya kutokea hitilafu uzalishaji maji ulikuwa katika kiwango cha chini kiasi cha lita milioni 170, hivyo kuathiri upatikanaji maji katika maeneo hayo.

"Nilikuwa katika ziara ya mkoa wa Simiyu, nikapata taarifa za kelele za malalamiko kuhusu kukosekana kwa maji hasa katika maeneo ya Malamba Mawili, Saranga, Mbezi Msakuzi, Bonyokwa na maeneo mengine, nikalazimika kumaliza ziara ili nije nijue tatizo ni nini," alisema Aweso.

Waziri huyo aliwashukuru mafundi wa DAWASA kwa kuhakikisha wanafanya kazi usiku na mchana kumaliza tatizo hilo ili wananchi waendelee kufurahia huduma ya maji.

Aliagiza wafanyakazi wa DAWASA pamoja na Wizara ya Maji kuhakikisha hawazizoei shida za wananchi, bali wahakikishe kuwa wanawapatia maji safi na salama kwa wakati kwa kuwa wakazi wa Pwani na Dar es Salaam hawana mbadala mwingine wa maji.

"Menejimenti msikae ofisini, maji hayana mbadala, hivyo DAWASA timizeni wajibu wenu, hatuna kisingizio kwamba maji katika mto yapo kidogo, maji yapo ya kutosha, tuwaombe wananchi radhi kwa hii hitilafu, piteni maeneo yote tusilete visingizio," alisema Aweso.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson Simon pamoja na kumshukuru Waziri Aweso kutembelea na kukagua mtambo huo, alisema kuwa hivi sasa wamewekeza zaidi kudhibiti mifugo kuathiri vyanzo vya maji.

"Tumeimarisha ulinzi kwenye mto wetu wa Ruvu, juzi tuliondoa zaidi ya mifugo 3,000 na tayari tumeshaandaa vyanzo vingine vya kunywesha maji mifugo yetu, lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wa Dar es Salaam na Pwani wanaendelea kupata maji safi na salama," alisema Nickson.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani, David Mramba, alisema wiki mbili zilizopita Wizara ya Maji ilituma wataalamu wake baada ya kuripotiwa hitilafu katika mtambo wa Ruvu Juu.



# Silayo awapa somo wafugaji nyuki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMISHNA wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS), Profesa Dos-antos Silayo, amewashauri wadau wa ufugaji nyuki nchini kujiandaa kimkakati kutumia Mkutano wa Dunia wa Ufugaji Nyuki (Apimondia) kujiinua kiuchumi na kuvutia watalii.

Prof. Silayo alitoa ushauri huo jijini hapa wakati wa mbio za nyuki zilizoshirikisha wanariadha 500 kutoka mataifa ya Afrika, Ulaya na Asia.

Mbio hizo zenye urefu wa kilometa 21 ni mahususi kwa ajili ya kuchagiza mkutano huo unaotarajia kufanyika mwaka 2027.

Alisema utunzaji wa mazingira utawezesha nyuki kuzaliana kwa wingi na kuwezesha uchumi kukua.

Aliwaomba wananchi kufunga nyuki kwa kutumia mizinga ya nyuki kwani nyuki ni mtaji na mazingira lazima yalindwe.

Rais wa Taasisi ya Nyuki Afrika, David Mukomana, ambaye ni raia wa Zimbabwe, alisema mbio hizo zina lengo la kutangaza mkutano huo.

Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Woker Bees Africa ( WBA), Restetuta Lazarus, alisema lengo la mbio hizo ni kuelezea umuhimu wa nyuki kwa maisha ya binadamu, umuhimu wake wa kutupatia chakula na asali ambayo ni tiba ya magonjwa.

Meya wa Jiji la Arusha, Maximilian Iranghe, alisema Mkoa wa Arusha umegawa mizinga ya nyuki milioni 2 katika mbio za Nyuki Marathoni huku 20 ikigawiwa kwa makundi mbalimbali.

"Tunataka Arusha iwe na nyuki wengi na dunia kwa ujumla, kutokana na utunzaji wa mazingira, hivyo mkutano wa Epimondia 2027 utakuwa chachu katika kuleta maendeleo," alisema.

Washindi katika mbio hizo wanawake, Nuru Benedicto, aliyetumia saa 1:21:59 na wanaume ni Mathayo Sombi kutoka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) 1:6:47.

# Tanzania yawakuna wabunge PAP

**Na Allan Isack,** LONGIDO

WABUNGE wa Bunge la Afrika (PAP) wameonyeshwa kuridhishwa jinsi Tanzania ilivyotatua migogoro ya mipakani na kuondoa vikwazo vya biashara dhidi ya nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Wajumbe hao wa PAP wameeleza kuwa kutokana na Tanzania kupiga hatua kwa kuondoa vikwazo hivyo, itaongeza wigo wa kufikia malengo ya kuwa na eneo la Biashara Huru kwa Bara la Afrika (AfCFTA).

Akizungumza katika Kituo cha Huduma cha Pamoja Mpakani (OSBP) kilichoko Namanga wilayani hapa Mkoa wa Arusha, Kiongozi wa Kamati ya Biashara, Forodha na Uhamiaji wa PAP, Profesa Margaret Kamar, alisema Tanzania imechaguliwa kuwa miongoni mwa nchi nane za mfano utekelezaji wa awali kufanya biashara huru.

Prof. Margaret, alizitaja nchi nyingine zinazotekeleza AfCFTA kuwa ni pamoja na Rwanda, Ghana, Mauritius, Cameroon na Tunisia.

Alisema lengo la ziara hiyo nchini ni kuangalia namna ya utoaji wa huduma maeneo ya mpakani ikiwamo wa Namanga.

Alisema baada ya kufanya ziara hiyo, wamejionea Tanzania ilivyojitahidi kuhakikisha suala la usalama mipakani linaimarika, ikiwamo utoaji na uingizwaji wa mizigo kupitia mashine za kisasa za ukaguzi.

Alisema ajenda kubwa iliyobebwa na bunge hilo ni kuhakikisha biashara huru inaimarika maeneo ya mpakani na kujionea namna zinavyofanyika na hatua zinazostahili hasa kwenye ukaguzi unaofanywa Namanga.

"Tumekuja kuangalia jinsi gani nchi ya Tanzania inavyotekeleza biashara huru hasa nchi za EAC, ikiwamo udhibiti wa bidhaa, tumeridhika na utoaji huduma nzuri katika mpaka huu na wa Namanga unaounganisha nchi ya Kenya na Tanzania," alisema.

Mbunge kutoka Bunge la Shelisheli, Wavel Woodcock, alisema Serikali ya Tanzania, imejitahidi katika sekta ya miundombinu maeneo ya mipakani na eneo la Biashara Huru katika ukanda wa nchi za EAC.

Mbunge wa Viti Maalum wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Anatropia Theonest, alisema mafanikio yaliyopatikana kwa Tanzania ni mengi.

Alisema wamepokea maelezo kutoka kwa wahusika wa mipakani ikiwamo uharakishwaji wa utoaji mizigo inayoingia na kupita kwenda nchi nyingine.

Alitayaja maelezo mengine waliyopokea ni pamoja na kukosekana kwa vitambulisho au vibali vya kuingia na kutoka nje ya nchi za EAC kwa wananchi wanaovuka mipaka kwenda nchi nyingine

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Salum Kali, alisema mikataba ya biashara kwa nchi wanachama wa jumuiya hiyo, ikiimarika wafanyabiashara watanufaika ikiwemo kuondoa vikwazo usafirishaji wa mizigo.

Kali, alisema vikwazo vikiondolewa itasaidia magari kukaguliwa haraka, kuondoka na kutumia vifaa maalum vinavyoweka maeneo ya mipakani.


SIMBA CEMENT
Heidelberg Materials

## CAUTIONARY NOTICE TO MEMBERS

### TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY (DSE: TCPLC)

(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)("Tanga Cement PLC")

1. Scancem ilinunua asilimia 68.33 ya hisa zote za Tanga Cement PLC ("Tanga Cement") kutoka kwa AfriSam Mauritius Investment Holdings Limited ("AfriSam"), ambazo kwa idadi ni hisa 43,504,403 (milioni arobaini na tatu laki tano elfu nne mia nne na tatu), kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Mauziano ya Hisa wa tarehe 22 Oktoba 2021 ("Mkataba wa Ununuzi wa Hisa au Mkataba").

2. Kwa mujibu wa Mkataba huo, malipo ya awali yaliyokubaliwa mnamo tarehe 22 Novemba 2022 ("Tarehe ya Awali"), baada ya kufanya marekebisho kadhaa, yalikuwa ni Dola za Marekani 42,492,369 (Dola milioni arobaini na mbili laki nne tisini na mbili elfu mia tatu sitini na tisa). Kiasi kilicholipwa ni sawa na Shilingi za Tanzania, TZS 106,383,896,028 (Bilioni mia moja na sita milioni mia tatu themanini na tatu laki nane tisini na sita elfu na ishirini na nane), ikiwa ni malipo ya awali ya Shilingi elfu mbili na mia nne arobaini na tano (TZS 2,445) kwa kila hisa.

3. Baada ya marekebisho ya bei ya awali, Scancem na Afrisam kupitia nyongeza kwenye Mkataba wa Ununuzi wa Hisa (addendum) wa tarehe 13 Septemba 2024, makubaliano yalifikiwa kwamba malipo ya mwisho ya ununuzi wa hisa ni Dola za Marekani milioni thelathini na tisa laki nne elfu tisini na mbili mia tatu sitini na tisa (USD 39,492,369). Kiasi hicho ni sawa na Shilingi za Tanzania TZS 98,873,095,028.40 (Shilingi bilioni tisini na nane milioni mia nane sabini na tatu elfu tisini na tano ishirini na nane na senti arobaini); ikiwa ni sawa na malipo ya Shilingi elfu mbili na mia mbili na sabini na tatu (TZS 2,273) kwa kila hisa.

4. Shilingi za Tanzania zimelinganishwa na Dola za Marekani na kunukuliwa katika aya ya 2 na 3 hapo juu kwa mujibu wa viwango vya ubadilishaji fedha za kigeni, USD kwenda TZS, kama ilivyokuwa katika Tarehe ya Awali; ilivyonukuliwa saa 8 mchana (2pm) kwa viwango vya ubadilishanaji fedha vya Bloomberg BFIX, ambayo ilikuwa sawa na fedha za Kitanzania Shilingi elfu mbili mia tano na tatu na senti sitini kwa Dola Moja ya Marekani (TZS 2503.60/1USD).

5. Scancem inawasiliana na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA au Mamlaka) ili kujua hatua zinazofuata kwa mujibu wa sheria na itatoa matangazo mengine huko mbeleni kama inavyotakiwa.

6. Tanga Cement ilishajulishwa kuhusu hitimisho la bei ya mwisho ya hisa na sasa itazingatia matakwa ya sheria na kanuni kadri itakavyoelekezwa na Mamlaka.

**Kuhusu Tanga Cement**


Tanga Cement ilisajiliwa nchini Tanzania mwaka 1980 kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ikiwa kampuni ya umma yenye dihima ya ukomo. Kampuni hiyo iko takribani kilomita 15 kutoka katikati ya Jiji la Tanga. Tanga Cement ina kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha klinka na saruji kwa kutumia chokaa inayopatikana katika eneo la kiwanda.

**Kuhusu Scancem**

Scancem ni kampuni-ubia iliyoanzishwa huko Norway katika mji wa Oslo mwaka 1986. Namba yake ya usajili ni 943 513 716 na anuani yake iliyosajiliwa ni: c/o Heidelberg Materials Norway AS, Lilleakerveien 2A, 0283 Oslo, Norway. Wabia wake ni kampuni mbili zilizosajiliwa Norway, kampuni zote mbili zinamilikiwa kwa asilimia 100 na Heidelberg Materials. Scancem ni sehemu ya wauzaji wakubwa wa vifaa vya mbao na vifaa vingine vya ujenzi na inazalisha, inauza na kusambaza simenti.

**Kwa niaba ya Bodi.**

Hakan Gurdal
**Mwenyekiti was Bodi**
21 Oktoba 2024



# Mzee adaiwa mahari baada ya mwanawe kutokuzaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Kitongoji cha Shilabela Kijiji cha Bugomba B, Kata ya Ubagwe, wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, Petro Sayi anadaiwa ng'ombe sita aliopokea mahari wakati akimuoza mtoto wake wa kike kwa kile kilichodaiwa ni kuishi na mumewe kwa miaka minne ya ndoa bila kupata mtoto.

Akisimulia mkasa huo juzi nyumbani kwake mbele ya wazee wa kimila walioshuhudia akipokea ng'ombe hao mwaka 2017 wakati akimuoza mtoto wake huyo akiwa na miaka 14, alisema uamuzi huo umeshtusha.

Sayui, alisema, mtoto wake huyo aliolewa na kuishi na mume wake katika Kata ya Nyankende-Ushetu kwa miaka minne na kwamba alishangaa mwaka jana amerudishwa nyumbani baada ya familia ya mumewe kudai wanamhitaji.

Alisema alirudishwa nyumbani hapo bila ya kuwa na mzigo, isipokuwa nguo alizokuwa amevaa.

Sayi, alisema alihoji sababu za kurejeshwa nyumbani na kujibiwa tangu aolewe hajawahi kuzaa wala kushika ujauzito, hivyo wampokee na kuombwa akabidhi ng'ombe hao mara moja.

"Nilikaa kimya na baada ya mwaka mmoja niliEetewa taarifa ya kuitwa mahakamani na kutolewa hukumu nirudishe ng'ombe saba kwa sababu mwanangu ametia hasara familia aliyoolewa kwa kuwa hazai, kama mahari ni zawadi iweje nirudishe au nilikuwa nimekopeshwa?" Alihoji Sayi.

Alisema hana uwezo wa kurejesha ng'ombe hao kwa madai kuwa mwanawe akiwa kwa mumewe, alikuwa anazalisha mazao shambani, kupeleka mifugo ya ukweni machungani na kuhudumia familia aliyokuwa anaishi nayo.

Sayi aliomba serikali kuingilia kati kwa kumaliza mgogoro huo ambao umeibuka baina yao.

Kwa upande wake, Anastazia Sayi, alithibitisha kuolewa akiwa na miaka 14 bila ya kulazimishwa na wazazi kwa kuwa alipenda kuwa na familia yake kama ilivyokuwa kwa wasichana wa rika lake kijijini hapo.

Anastazia, alisema mpaka anarejeshwa nyumbani kwa wazazi wake hakubahatika kupata mtoto.

Alisema mwanzoni maisha ya ndoa yao na mumewe yalikuwa mazuri, mwaka mmoja baadaye yalibadilika na kuanza kuteseka kwa kutumikishwa kazi za kiume, ikiwamo kuchunga mifugo hiyo kwa amri ya mama mkwe wake.

Alisema mama mkwe wake alikuwa akimlazimisha mumewe amrejeshe nyumbani kwa wazazi wake na kuoa mwanamke mwingine wa kumzalia watoto huku akimsisitiza ahakikishe mahari yao inarejeshwa.

Alidai mpaka mumewe anamrejesha kwao alikuwa tayari ameoa mwanamke mwingine mwenye watoto watatu.

"Licha ya kusema sina uwezo wa kupata mtoto, lakini hatujawahi kupima kujua ni nani mwenye tatizo kati yangu au mume wangu kwani hata huyo aliyekutana naye akiwa na watoto, mpaka sasa hajapata mtoto pia," alidai Anastazia.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho aliyemaliza muda wake hivi karibuni, Msafiri Hussein, amethibitisha kupokea malalamiko ya familia hiyo.

Hussein, alisema kabla ya kuchukua hatua ya kuziita familia hizo mbili, walipata wito wa kuitwa mahakamani.

Alisema awali familia hiyo ilikubali kutoa ng'ombe wawili au kiasi cha Sh.200,000, kwa kila mmoja Sh.100,000, lakini mahakama ilisikiliza kesi na kuamuru kurejesha wote sita.

Mama mkwe wa Anastazia, Lusia Lushinge alithibitisha kumrejesha nyumbani mkewe huyo na kudai ng'ombe hao kwa kukosa mjukuu.



Wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wilayani Nzega, mkoani Tabora wakichuja mchanga ili kutafuta madini hayo. Wameshauri serikali kuzuia matumizi ya kemikali ya zebaki katika shughuli hizo baada ya kubaini athari zake kwa afya na mazingira. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Wananchi watakiwa kudumisha amani

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

WANANCHIi wametakiwa kulinda na kudumisha amani nchini katika kipindi cha uchaguzi.

Rai hiyo ilitolewa juzi na kiongozi wa huduma ya matengenezo ya kiroho ulimwenguni, Augustine Tengwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa kuhusiana na uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu mwakani.

Tengwa, alisema ili kudumisha amani ni vyema wanasiasa wakakubali matokeo yatakapotangazwa na kuepuka uchochezi.

"Tusipoilinda amani ya nchi yetu kama mabaya yatatokea kama yaliyotokea nchini jirani, tutaenda wapi,“ alisema Tengwa na kusisitiza kuwa:

"Wakati wa uchaguzi wanasiasa naomba ukishindwa nyamaza kimya usianze kutafuta vikundi vya vijana kuleta uchochezi."

Alisema suala la kuwa kiongozi ni mpango wa Mungu na ni pekee mwenye mamlaka ya kuamua nani atawale na kwa wakati gani.

Mtumishi, Agnes Bruno alitoa tahadhari kwa wagombea kuisikia sauti ya Mungu na kuzingatia.

## Nyangwine azipatia sekondari vitabu

**Na Samson Chacha,** TARIME

MWANDISHI na vitabu nchini, Nyambari Nyangwine ametoa vitabu vya kiada bure kwa shule za sekondari za Halmashauri za Tarime Mjini na Vijijini Mkoa wa Mara vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100 ili kuboresha elimu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari wilayani hapa kuhusu usambazaji wa vitabu hivyo, Msemaji wa Taasisi ya Nyambari Nyangweni (NNF), Jacob Mugini, alisema lengo ni kuunga mkono serikali kuhakikisha wanafunzi wanapata zana za kujifunzia.

Mugibi, alisema vitabu hivyo ambavyo vimetolewa na taasisi hiyo vya kiada ni pamoja na vya Hisabati, Jiografia, Sayansi na Historia.

Alisema vitabu hivyo vya masomo hayo kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, vitasambazwa wakati wowote katika shule hizo.

Taasisi hiyo hadi mwaka 2020 ilitoa bure vitabu vya kiada vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200 kusaidia kuinua kiwango cha elimu nchini.





Ukurasa 13

Maelfu wanafunzi kufikiwa kampeni ya 'Safari Bila Rushwa Ngono Inawezekana'

Nipashe

# TESA

Jumanne Oktoba 29, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

HATARI; JOTO, MIONZI, SUMU...

## Wazalishaji nyuklia Ulaya wahangaika kubuni dampo la handaki wasidhurike

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Maagizo ya Rais yajibu mazito katika matamasha ya Utamaduni, Majimaji

- Aelekeza yawe ya kibiashara, kote nidhamu ya mila
- Wizarani wabuni vituo 100 vya Kiswahili diaspora



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akikagua Makumbusho ya Songea, alipotembelea Tamasha la Majimaji, mwezi uliopita. **PICHA MTANDAO**

NI wastani wa mwezi mmoja sasa kuna matukio makuu kitaifa na kimataifa yanayobeba sura ya historia, pia utalii wa nchi, ambayo yamefanyiwa sherehe maalum.

Hapo kunatajwa matamasha ya utamaduni kitaifa katika jozi na linalokukumbuka miaka 119 tangu kutokea vita vya Majimaji nchini, sasa pakibaki historia inayoipa nchi heshima na mvuto mkubwa wa taifa kitalii.

Wakati rekodi ya Tamasha la Vita Majimaji likiwa mara ya 10, kwa Tamasha la Utamaduni, ufafanuzi wake anautoa Naibu Waziri wa Waziri wa Sanaa, Michezo na Utamaduni, Hamisi Mwinjuma maarufu 'Mwana FA', Juni mwaka huu, akieleza:

"Rais (akiwa Mwanza 2021) aliagiza kufanyike kwa Tamasha la Utamaduni kila mwaka, ili kurithisha mali na utamaduni wa kitanzania..."

Pia, ni hivi karibuni nchini kulikuwapo ugeni mkubwa kutoka Ujerumani, taifa lililokuwa mahasimu vitani, wakienzi na kujutia yaliyojiri katika vita vya Majimaji, nao wakizuru mkoani Ruvuma kwa heshima ya kipekee.

Katika matukio ya mkoani Ruvuma, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mwanasheria Dk. Damas Ndumbaro, ndiye mwenyeji wake kipindi chote, akiwa kwenye jimbo analowakilisha, pia wizara yake ni mdau mwenye dhamana ya tukio

Ulipofika ugeni wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ziarani mkoa wa Ruvuma, akijumuisha safari na ukaguzi wa maendeleo Kusini na Nyanda za Juu Kusini mwezi uliopita, akatembelea Makumbusho ya Vita vya Majimaji yaliyoko mjini Songea.

Hapo kukafafanuliwa lengo mahsusi kwa Rais kutembelea mahali hapo Makumbusho, ilikuwa kutoa heshima ya Kumbukizi ya Mashujaa wa Vita ya Majimaji vilivyopiganwa kuanzia mwaka 1905 mpaka 1907.

Viongozi wenyeji waliompokea wamo wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakiongozwa na Waziri Balozi Dk. Pindi Chana, Katibu Mkuu, Dk. Hassan Abbas na Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Noel Lwoga.

Nao wakaambatana na uongozi wa mkoa wa Ruvuma, Chifu wa Wangoni - Zulu Gama I, wazee wa mila, pia dini mkoani.

Mzunguko wake Rais kwenye Ukumbi wa Historia ya Vita ya Majimaji, ukafikia Onyesho la Nyumba ya Inkosi (Chifu) wa kabila la Wangoni, alikoweka shada la maua katika Kaburi la Halaiki la Mashujaa 66 wa Vita ya Majimaji na Kaburi la Chifu Msaidizi (Nduna Songea Luwafu Mbano.

Historia iliyoko ni kwamba, vita vya Majimaji mizizi yake inaanzia eneo la Nandete Kipatimu, mkoani Lindi, ambako jamii la kabila la Matumbi zikajitokeza kwa ujasiri dhidi ya ukandamizaji huo wa kikoloni.

Hisia hizo za upinzani zikachochea moto ulioenea hadi Ruvuma, ambako nako umma ukichochewa na ujasiri wa majirani zao, wakaanza kuungana katika mapambano yao, dhidi ya uhasimu huo, wakiziharibu barabara walizolazimishwa kujenga.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbasi, akifunga sherehe hiyo ya kuadhimisha miaka 119 ya Vita ya Majimaji eneo la Nandete, Kata ya Kipatimu, Kilwa mkoani Lindi, anamsifu Rais Dk. Samia kuenzi mchango wa wapigania uhuru, ikiwamo historia ya vita vya Majimaji.

"Wazee wetu walioongoza vita vile chini ya Jemedari Mkuu Mzee Kikwako Mbonde na mwa-

INAENDELEA UK.12

# Maagizo ya Rais yajibu mazito katika matamasha ya Utamaduni, Majimaji

INATOKA UK.11

nafalsafa wake mkuu na mhamasishaji Mohammed Ali Kinjekitile Ngwale, walipandikiza mbegu ya ari ya uhuru na uzalendo ambayo leo Rais wetu Dk. Samia Suluhu anaienzi kwa kuleta maendeleo.

"...serikali yake (Dk.Samia) imeyatangaza rasmi kupitia GN 163 na 166 maeneo ya Nandete yaliyohusika na vita hiyo kuwa urithi wa Taifa na Kimataifa," anatamka Dk. Abbas.

Mbali na viongozi wa kiserikali, pia maadhimisho hayo yalihudhuriwa familia za wapigania uhuru hao na mamia ya wananchi ambayo Dk. Abbas akaahidi kumwomba Rais Samia mahali hapo pajengwe Makumbusho Maalum ya Vita vya Majimaji.

Katika maadhimisho hayo, wadau mbalimbali wamechangia vitu na kuahidi vyakula zikiwamo kilo 1,500 za mchele, itakapotimu miaka 120.



Dk. Samia Suluhu Hassan, akikagua aina ya vyakula vya kimila. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

#### TAMASHA UTAMADUNI

Wakati awali akitangaza kilichotarajiwa kuajiri katika Tamasha la Utamaduni mwaka huu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa akaahidi lingekuwa na mitazamo mikuu sita, akiitaja ni:

Mirindimo ya kiasili kuanzia mavazi, maonyesho, visasili na visakale; mdahalo wa kitaifa kuzungumzia mapambano dhidi ya viashiria vya mmomonyoko wa maadili na mchango wa jamii katika kupunguza na hatimaye kuondoa viashiria hivyo.

Eneo lingine ni onyesho maalumu la matumizi ya khanga ikiwa vazi la utamaduni wa Mtanzania; pia vikundi 25 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar; vikundi sanaa ya asili, ubunifu, utamaduni na muziki wa kizazi kipya.

Aidha, kukatajwa mashindano ya uhifadhi wa ngoma za asili kwa vikundi 25 vya Tanzania Bara na Visiwani na kliniki ya sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Katika hilo, Naibu Waziri Mwinjuma anatamka: "Tanzania ina utajiri wa makabila zaidi ya 120, tofauti yake inajenga umoja na yanaunganishwa na lugha ya Kiswahili....

"Kudumu kwa Utamaduni inategemea namna inavyorithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine na kwamba urithi wa utamaduni ni kivutio kikubwa cha utalii, watalii wamevutiwa sana."

#### TAMASHA IWE BIASHARA

Akifunga tamasha hilo Septemba 23 mjini Songea, Rais Dk. Samia, akatoa rai kwa wananchi na wadau wa sekta za utamaduni na utalii, kuufanya utamaduni kuwa biashara, ulete manufaa ya

> "Kudumu kwa Utamaduni inategemea namna inavyorithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine na kwamba urithi wa utamaduni ni kivutio kikubwa cha utalii, watalii wamevutiwa sana.



Ni sehemu ya ziara, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitoka katika nyumba ya mfano kwenye Tamasha la Utamaduni, Songea mwaka huu.

kiuchumi kwa nchi.

Anataja madhumuni ya matamasha ya utamaduni yanayofanyika nchini, ni kuendeleza, kuenzi na kulinda utamaduni na mila za nchi, pia kufungua fursa za kiuchumi kwa Watanzania kupitia kazi za sanaa na utamaduni.

Kuhusu lugha ya Kiswahili, Rais Dk. Samia anasema, ni vigumu kwa Tanzania kujadili utamaduni wake, pasipo kugusa lugha anayotumia- Kiswahili, inayowaunganisha wananchi, hata kuwafanya kuwa na utamaduni mmoja.

Kwa mujibu wa Rais, ni mazingira yanayofungua fursa mpya za kiuchumi na kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, serikali imejipanga kufungua vituo vya lugha 100 vya Kiswahili, kwa kushirikiana na diaspora kote duniani.

Anayeelekeza suala la mmomonyoko wa maadili kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ushirikiano na taasisi na wadau mbalimbali kulifanyia kazi suala, ili kuja na mapendekezo ya namna bora ya kulishughulikia.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas, akaitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuwachukulia hatua kali wote wanaohujumu mila na desturi za nchi kwenye mitandao ya kijamii.

"Ili Taifa liwe hai, lazima tuenzi na kuendeleza utamaduni wetu, na lazima turithishe utamaduni wetu kwa vijana na watoto na lazima tuwafundishe watoto wetu mila na desturi za Kitanzania, Kiswahili. Tuwafundishe miiko mbalimbali na historia yetu kwa kuwa hawa watoto ni taifa la kesho," anahimiza.

Anaendelea:"Sasa hivi duniani kuna suala linaitwa haki za binadamu. Ni jambo linalopaswa kuliheshimu na kulizingatia, lakini tusitumie haki za binadamu kuingiza utamaduni wa kigeni zisizofaa katika jamii yetu.

"Taasisi za elimu kuanzia chekechea hadi chuo kikuu ni muhimu kurithisha utamaduni wetu una mila zetu katika kupambana na mmomonyoko wa maadili.

"Tuwafundishe maadili mema watoto wetu, viongozi wa dini mna kazi kubwa sana na maadili mengi ya dini yanatusaidia kulinda utamaduni wetu," anasema Dk. Ndumbaro.

Akakumbusha kuwa mnamo Septemba 8, 2021 katika maadhimisho ya utamaduni wa Bujora mkoani Mwanza, Rais Samia Hassan Suluhu alitoa maelekezo kwa wizara hiyo kuandaa tamasha la kitaifa litakalofanyika kila mkoa.

"Maelekezo yale yametufanya tuwe Songea leo, uwepo wetu hapa ni maelekezo ya Rais Samia kudumisha tamaduni zetu," anasema, akitaja Tanzania imebarikiwa kuwa na makabila zaidi ya 120 na lugha za kijamii zaidi ya 150 na ni utajiri wa kiutamaduni.

"Utamaduni wetu unategemea nguzo zifuatazo moja ni upendo, mshikamano, umoja, amani na utulivu, yote tunayoyafanya ili kuendeleza nguzo hizi," anasema.

#### WAZIRI UTALII

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi, anasema, serikali inaendelea kushirikiana na jamii kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni, ikiwamo ujenzi na ukarabati wa nyumba za asili za Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam.

Akizungumza katika tukio la Tamasha la Utamaduni la Watu wa Kigoma, mwezi uliopita, Dar es Salaam, Waziri akasema: "Ni dhahiri kwamba kwa mashirikiano haya ya serikali na wanajamii ya mkoa wa Kigoma katika tamasha hili hapa Kijiji cha Makumbusho."

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Makumbusho ya Taifa, Dk. Oswald Masebo, anasema Tamasha la Siku ya Utamaduni wa Mtanzania ni la 30 tangu kuanzishwa mwaka 1994.

Ni takribani makabila zaidi ya 37 nchini ambayo yamefanya maonyesho yao tangu kuanzishwa utaratibu huo, kati ya makabila zaidi ya 120 yaliyopo nchini.

Tamasha hilo lilipambwa na ngoma za asili, nyumbani, vyakula na vinywaji, mavazi ya asili.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Maelfu wanafunzi kufikiwa kampeni ya ‘Safari Bila Rushwa Ngono Inawezekana’

KAMPENI ya ‘Safari Salama Bila ya Ngono Inawezekana’ inayolenga kuwajengea wanafunzi uelewa, kuhusu madhara ya rushwa ya ngono imeingia awamu ya sita, ikitarajiwa kufikia wanafunzi zaidi laki moja.

Elimu hiyo pia inawahusu madereva wa bodaboda, bajaj na daladala ili nao waweze kushiriki kikamilifu katika vita hiyo, kwa kuwa wao ni miongoni mwa watuhumiwa wa rushwa ya ngono.

Wanaoendesha kampeni hiyo ni Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), kwa kushirikiana na wadau wake ambao ni madereva wa bodaboda, bajaji na daladala.

Pia, wamo viongozi wa manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke mkoani Dar es Salaam, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na walimu wa shule za msingi na sekondari.

Hivi karibuni, WAJIKI ilizindua kampeni hiyo ya awamu ya sita eneo la Bunju A, Dar es Salaam na sasa inaendelea kwa nyakati tofauti katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke, huku ikitarajiwa kudumu kwa miaka miwili.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, anasema kampeni hiyo itasaidia kuwajengea uwezo pia madereva ili wajue umuhimu wa kumlinda mtoto wa kike dhidi ya rushwa ya ngono.

“Kuna kata mpya ambazo tutatoa elimu kwa mara ya kwanza ambazo ni Bunju A wilayani Kinondoni, Kitunda wilayani Ilala na Kibonde Maji wilayani Temeke. Katika kata hizo, kila moja tutafikia wanafunzi 35,000, walimu 100, madereva 200,” anasema Janeth.

Janeth anafafanua kuwa jumla ya kata hizo tatu, watafikia wanafunzi zaidi ya laki moja, walimu 300 na madereva 600, ili kuwajengea uwezo wa kutambua madhara ya rushwa ngono na jinsi ya kuwalinda wanafunzi na watoto wa kike kwa ujumla.

Anaahidi watafika katika shule nne za msingi na mbili za sekondari kwa kila kata, huku wakitoa elimu kwa njia ya mikutano ya wazi shuleni, vijiwe vya bodaboda, bajaji, daladala na pia kwenye masoko.

Mbali na kutoa elimu ya kupambana rushwa ya ngono, anasema watakuwa wanahamasisha wanawake kujitokeza kwa wingi kuwania uongozi kwenye uchaguzi wa mwaka 2025.

“Women Fund Tanzania Trust (WFT-T), wamefadhili kampeni hii kwa Sh. milioni 800 kwa muda wa miaka miwili kufikisha elimu hii kwa wanafunzi na kwenye makundi mengine,” anasema.



Wadau katika maandamano ya uzinduzi wa kampeni ya ‘Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana’ Kata ya Charambe, Mbagala Dar es Salaam. **PCHA ZOTE: SABATO KASIKA**



Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, akizungumzia kampeni, Mbagala Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Katika ufafanuzi wake, anasema watakuwa wanafanya kampeni na kupumzika kwa ajili ya tathmini ili kuona ni wapi wamefanikiwa na wapi penye changamoto ili warekebishe kabla ya kuendelea hadi utumie miaka miwili, na kwamba wanaandaa ratiba huku tukiendelea na kazi.

Aidha, anasema awamu tano zilizopita za kampeni hiyo, walifika katika shule 28 wilayani Kinondoni. zikiwamo sita za sekondari, huku wilayani Ilala wakiwa wamefika katika shule nne za msingi na tatu za sekondari.

“Katika Wilaya ya Temeke tulifika shule tatu za msingi na tatu za sekondari. Awamu hii ya sita tutafika katika shule sita zikiwamo nne za msingi, wilayani Temeke ambako ndiko tunaanzia kampeni yetu baada ya uzinduzi uliofanyika kule Bunju A,” anasema.

> Women Fund Tanzania Trust (WFT-T), wamefadhili kampeni hii kwa Sh. milioni 800 kwa muda wa miaka miwili kufikisha elimu hii kwa wanafunzi na kwenye makundi mengine.

### KIKWAZO KIKO HUKU

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Kinondoni, Furaha Dibango, anasema manispaa hiyo inashirikiana na WAJIKI katika utoaji wa elimu, lakini anadai kuwa baadhi ya wazazi na walezi ni kikwazo.

Anaweka wazi kuwa ni muda mrefu tangu WAJIKI waanze kutoa elimu hiyo imesaidia watoto kuwa na uelewa wa kutosha na wanatoa taarifa za ukatili wanaofanyiwa majumbani na mitaani.

“Taarifa za ukatili zinatolewa, tunafuatilia na kubaini ukweli na kufikisha matukio katika vyombo vya sheria, lakini wazazi na walezi wanapoitwa kutoa ushahidi huwa hajitokezi,” anasema Furaha.

Anasema badala yake wamekuwa wakimalizana na wahalifu kimya kimya na kuongeza kuwa mtindo huo unakwamisha vita ya rushwa ya ngono na ukatili mwingine unaoendelea kutokea ndani ya jamii.

Anataja baadhi ya ukatili huo ambao wazazi na walezi wanakwepa kuutolea ushahidi kuwa ni ubakaji, mimba za utotoni, ulawiti, huku akiongeza kuwa ni wa kukemewa na kila mzazi, mlezi na jamii.

Hivyo, wito wangu kwa wazazi na walezi ni kwamba, watoe ushirikiana kwa vyombo vya sheria ili wanaojihusisha na ukatili wachukuliwe hatua badala ya kukaa pembeni na kusababisha vitendo hivyo kuendelea.

“Ni aibu mzazi au mlezi kukubali kupokea chochote kutoka kwa mtuhumiwa kwa lengo la kuficha ukweli, kwani hatua hiyo inaacha kovu moyoni mwa yule aliyefanyiwa ukatili,” anasema.

Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoa wa Kinondoni, Bibie Msumi anasema, mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika vita ya rushwa ya ngono imeongeza uelewa wa jamii kutoa taarifa za matukio ya ukatili huo.

“Kwa sasa jamii imepata uelewa wa kutosha kupitia elimu inayotolewa na shirika hili na wadau wengine wanaopinga rushwa, kwani tumekuwa tukipokea taarifa nyingi za matukio hayo ambazo zinatusaidia katika majukumu yetu ya kila siku,” anasema Bibie.

Pia, anaongeza kuwa rushwa yoyote ile haifai kufumbiwa macho, akikwemea ‘wanaomalizana na wahalifu’, kutaka wazazi na walezi kutimiza wajibu wao wa maalezi bila kujihusisha na upokeaji wa kitu chochote kutoka kwa wahalifu, kwa kuwa watatingia katika mtego.

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

HATARI YA JOTO, MIONZI, SUMU...

# Wazalishaji nyuklia Ulaya wahangaika kubuni dampo la handaki wasidhurike

• Roboti zaandaliwa kupokea taka na kufukia



Picha za mahandaki ya kuhifadhi taka za nyuklia katika ujenzi, ya juu ni Finland na chini, Ufaransa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

SUALA la kuunda silaha za nyuklia ndio zimetawala kila kona za mataifa makubwa duniani. Hata hivyo, upande wa pili zinapigwa vita kimataifa, maana matumizi yake yana madhara makubwa kwa uhai, mazingira, kijamii, hata uchumi duniani. Kwa kifupi ni sumu.

Vilevile, inaelezwa taka za nyuklia hubaki kuwa sumu kwa maelfu ya miaka. Hivi sasa wazalishaji wake kutoka mataifa ya Ulaya kama Ufaransa, Uingereza, Finland, Sweden na Ufaransa, zimeanza kubuni mbadala wa namna ya kuzitupa.

Kinachofanyika sasa, kunachimbwa mashimo ya kina wastani wa futi 1,500 au sawa na mita 450, huko Ufaransa wakiwa wamechagua chini ya vilima vya eneo la Champagne, Kaskazini Mashariki mwa nchi hiyo, maeneo yanakochongwa kihandisi kuzika baadhi ya taka husika.

Hadi sasa kumeteuliwa eneo la mbali kufukia sumu hiyo, ambako mtu anatakiwa aendeshe gari kwa saa nne kutokea Mashariki mwa jijini Paris. Mahali husika kuna urefu wa kilomita 2.4 za mahandaki ambayo ni maeneo ya majaribio kisayansi, kukiwapo ujenzi na ubunifu wa kiteknolojia katika kuhifadhi sumu hizo.

Kuna kampuni ya taka za nyuklia ya Ufaransa, Andra inayohitaji kuthibitisha kituo hicho cha kuhifadhi ni salama kabla ya kupewa leseni. Ili kupata maeneo yanayoendana na mahitaji ya kuhifadhi taka hizo, huwa inabaki kuwa changamoto, hasa kwa usalama wa wakazi jirani.

"Utoaji leseni kwa vituo hivyo vya utupaji taka huchukua zaidi ya miaka 20 hadi 30," anasema Jacques Delay, mwanasayansi katika kituo hicho nchini Ufaransa.

"Kutupa taka kutadumu kwa takriban miaka 100 kabla ya kufungwa. Baada ya hapo, kutakuwa na mamia ya miaka ya ufuatiliaji wa eneo hilo," anaongeza.

Nchini Finland nako kitaalamu kunaelezwa kuwapo mahali penye maeneo ya kujenga na kuhifadhi taka za nyuklia kwa sababu hakuna matetemeko ya ardhi.

Nchi hiyo ilikuwa ya kwanza duniani kujenga kituo kirefu cha chini ya ardhi cha utupaji taka ya nyuklia za mafuta yaliyotumika na sasa imeingia katika hatua ya kwanza ya majaribio ya uwekaji taka hizo.

> "Kutupa taka kutadumu kwa takriban miaka 100 kabla ya kufungwa. Baada ya hapo, kutakuwa na mamia ya miaka ya ufuatiliaji wa eneo hilo.



Huko Ulaya Sweden, hadi sasa kazi ya ujenzi inakaribia kuanza, ambako ni mwendo wa saa mbili kwa gari, Kaskazini mwa jijini Stockholm, kwenye kituo kama hicho kinachotarajiwa kujengwa.

Nchini Uingereza, eneo la hifadhi kama hilo, penye mahandaki makubwa, nako ni mahsusi kuhifadhi taka nyingi za mionzi na kwa muda mrefu zinazalishwa na nyuklia.

Kwa ujumla barani Ulaya, taka hizo sasa zimehifadhiwa usoni mwa dunia katika vituo kama kile cha Sellafield nchini Uingereza na La Hague nchini Ufaransa.

Uchafu huo unatajwa kujumuisha vifaa vya vinu vya nyuklia, kemikali za kaboni kutoka katika kinu, mafuta na maji maji kutoka katika mafuta yaliyotumika kutoka vinu vya nyuklia.

Wataalamu huchunguza, iwapo eneo kama lina miamba chini ya ardhi wastani wa mita 500 hadi kilomita moja, kama kunafaa kuweka taka za nyuklia kwa zaidi ya miaka 100,000.

Nchini Finland mtaalamu, Pasi Tuohimaa, wa kampuni ya utupaji taka za nyuklia ya Finland, anasema: "Tumekuwa tukitengeneza umeme wa nyuklia tangu mwishoni mwa miaka ya 70."

### HALI YA MIGODINI

Migodi ya madini inatajwa haikujengwa kwa usahihi kuhifadhi taka za nyuklia, kwani kuna hatari nyingine, kwenye rasilimali za madini na hatari ya watu kuendelea kuchimba.

Pia, inatajwa mbinu bora ya kujenga kituo kipya cha madhumuni ya taka za nyuklia, mkakati wake unakuwa rahisi maana mkakati wake unaanza tangu hatua ya awali, tofauti na uamuzi wa sasa.

Kitaalamu inaelezwa kwamba, taka za viwango vya kati hutajwa kutoa joto kidogo na hivyo zinaweza kuhifadhiwa kwa usalama; huku taka za kiwango cha juu cha nyuklia, huzalisha joto zaidi na zinalazimika zihifadhiwe kwa kiasi kidogo, zikikaa mbalimbali.

Pia, inashauriwa kwamba, maeneo hayo ya kuhifadhi taka yanapaswa kuwekewa vizuizi kuzuia mionzi kutoka nje, vinavyoweza kujumuisha vyombo vya kuhifadhi na miamba inayoizunguka.

### NJIA ZAKE ZILIVYO

Wahandisi wa nchini Ufaransa, wameunda njia panda mbali ya kilomita nne (maili 2.5) ili kudhibiti usalama.

Ili kufikisha uchafu huo mahali husika, mkakati ni kunawekwa kitendea kazi aina ya roboti itakayotumika kusogeza mitungi ya taka katika mahali husika, ambalo linathibitika halina tetemeko la ardhi.

Nchini Sweden, mipango yake inafafanuliwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa SKB, Anna Porelius shirika linalodhibiti taka za nyuklia, kauli yake ni kwamba:

Inatajwa kwamba uwekaji taka za nyuklia utafanywa na mashine iliyoundwa maalumu inayoweza kuendeshwa kwa mbali kwa ufanisi.

Ni mashine itakayotumika kuweka mikebe ya shaba kwenye mashimo ya mita 500 (futi 1,650) chini kwenye mwamba.

Pia, inafafanuliwa kwamba teknolojia hubadilika, hivyo ni lazima kutengenezwe kituo kinachoweza kurekebishwa, kubadilishwa na kustahimili kwa muda mrefu utyunaji taka hizo.

Suala la uhifadhi wa nyuklia, miradi hiyo inafafamuliwa kwamba itachukua miaka mingi.

Mkurugenzi wa Mawasiliano huyo, anasema "hakuna hata mmoja wetu anayeweza kuona mradi wa hifadhi ya taka za nyuklia ukikamilika, lakini kile tunachofanya sasa ni suluhisho la taka za nyuklia kwa faida ya vizazi vijavyo. Kufanya hivyo... kunatupa motisha ya kusonga mbele."

• ***Kwa mujibu wa BBC***



# Waziri Silaa awafunda wafanyakazi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, amewataka watumishi mkoani hapa kutanguliza maslahi ya wananchi mbele katika utendaji wao ili kuchochea maendeleo.

Akizungumza na watumishi wa sekretarieti ya Mkoa wa Singida juzi mjini hapa, Silaa aliwaonya watumishi hao kuwa iwapo watatanguliza maslahi yao mbele badala ya wananchi kazi hazitakwenda vizuri jambo ambalo serikali haitegemei litokee.

"Tukiweka maslahi ya hapa Singida mbele kazi zitakwenda vizuri na tutaendelea kujenga taifa letu, niendelee kutoa wito tuchape kazi kwa kasi zaidi na pia tuyatangaze maendeleo makubwa yanayofanywa na serikali ili wananchi wayafahamu, " alisema.

Silaa, alisema katika kipindi cha miaka mitatu na nusu kwa mkoa huo, serikali imeleta fedha nyingi kutekeleza miradi ya maendeleo, hivyo ni jukumu la watendaji kuhakikisha wanasimamia fedha hizo ili iweze kukamilika kwa wakati na ubora.

"Rais (Samia Suluhu Hassan) hajaleta fedha hizi kuja kukaa kwenye akaunti, hakikisheni zinatumika kwenye miradi na msimamie ipasavyo, " alisema.

Akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Puma, aliwataka kuzingatia masomo kwani serikali imewajengea shule nzuri zenye mazingira mazuri ya kusoma.

"Sisi tunaoongea hapa shule tulizosoma hazikuwa katika mazingira mazuri, lakini leo hii sisi ni viongozi. Nawaomba someni sana serikali inawapenda ndio maana imejenga shule nzuri ili msome," alisema Silaa.

Akiwa katika kiwanda cha mafuta ya alizeti cha Wild Flower Grains&Oil Mill Company Limited kilichoko Manispaa ya Singida, alisema ni wakati wa Tanzania kupunguza kuagiza bidhaa nje ya nchi kwani maendeleo ya viwanda yatarahisisha uchakataji na upatikanaji wa bidhaa mbalimbali ikiwamo mafuta ya kula.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, aliwakaribisha wawekezaji katika mkoa huo, akisema ni mahali salama na una upatikanaji wa umeme na mazao ya biashara kama vile alizeti na vitunguu.

## Watakiwa kuiunga mkono serikali

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WADAU wa elimu, wazazi na walezi wametakiwa kuiunga serikali kutatua kero sekta ya elimu ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki na kufanya vizuri kitaaluma.

Rai hiyo ilitolewa na mdau wa maendeleo ya elimu mkoani Dodoma, Eva Mpagama baada ya kukabidhi mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Shule ya Sekondari Miyuji jijini hapa kwenye mahafali ya 16 ya kidato cha nne.

Eva, alisema wadau wa maendeleo wakishirikiana na wazazi na walezi, watasaidia serikali kutatua baadhi ya kero na kuharakisha maendeleo.

"Bado tuna nafasi kubwa ya kusaidiana na serikali kuondoa kero nyingi zilizopo kwenye shule zetu kuanzia za msingi na sekondari, tusisubiri Rais Samia Suluhu Hassan atatue hata sisi tunatakiwa kuunga mkono juhudi hizo," alisema.

Mkuu wa shule hiyo, Zubeda Salim, alisema baada ya kupokea msaada huo, wataanza ujenzi wa uzio huo kutokana na mazingira ya shule kuhatarisha usalama wa wanafunzi.

Salim, alisema shule hiyo inakabiliana na tatizo la utoro na mwingiliano wa watu kwa kipindi chote hali ambayo inayowafanya wanafunzi na walimu kukosa amani na utulivu.

Alisema pia wanakabiliana na upungufu wa matundu ya vyoo hayatoshelezi idadi ya wanafunzi iliyoko.



Mkuu wa Shule ya Sekondari Miyuji, jijini Dodoma, Zubeda Salim (wa pili kulia), akipokea risiti ya mifuko ya saruji 100 kutoka kwa mdau wa maendeleo ya elimu mkoani Dodoma, Eva Mpagama, kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule hiyo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wawakilishi watinga makao makuu e-GAZ

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

KAMATI ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imeitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kushirikiana na Mamlaka ya Zanzibar (e-GAZ) kusaidia maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) visiwani humo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machano Othman Said, alitoa wito huo wakati wa ziara ya kamati mwishoni mwa wiki iliyopita katika Makao Makuu ya e-GA jijini hapa.

Said, alisema e-GA imekuwa na mafanikio kwenye utekelezaji wa afua za serikali mtandao, hivyo ni muhimu kuwa na ushirikiano wa karibu ili kuchochea matumizi ya TEHAMA visiwani humo kukuza uchumi.

"Ndomba (Mkurugenzi Mkuu wa e-GA) tunaomba utusaidie kwenye hili, e-GAZ bado ni changa, tunahitaji Zanzibar nayo iingie kwenye matumizi ya kidigiti, tunahitaji kufika hadi kwa masheha wote watumie mifumo ya TEGHAMA katika shughuli zao za kila siku," alisema.

Alitoa wito kwa taasisi hizo za umma kutumia mifumo ya TEHAMA inayotengenezwa na Mamlaka za Serikali Mtandao nchini ili kuendeleza utawala bora, kudhibiti mapato ya serikali na kulinda usalama wa nchi katika zama za sayansi na teknolojia.

**Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machano Othman Said, alitoa wito huo wakati wa ziara ya kamati mwishoni mwa wiki iliyopita katika Makao Makuu ya e-GA jijini hapa.**

"Kama hakutakuwa na matumizi ya mifumo rasmi inayosomana itakuwa ni ngumu kuonesha mapato, matumizi na manunuzi katika taasisi za umma, hivyo nchi inaweza kupoteza mapato," alisema.

Alisema serikali imeonesha utayari wa mageuzi ya TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za kila siku kuwahudumia wananchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Zanzibar, Ali Suleiman Ameir, alisema lengo la ziara hiyo ni kujifunza hatua muhimu zilizofikiwa na e-GA kusimamia, kuratibu na kukuza jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma nchini.

Kwa upande wake Ndomba, aliahidi kuendelea kuimarisha ushirikiano na e-GAZ ili kuhakikisha serikali mtandao inaimarika kwa Bara na Visiwani na kuboresha utoaji wa huduma za serikali kwa wananchi.



# EU yawapa ahueni wakulima wa chai

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHILINGI milioni 224 zimetolewa na Jumuiya ya Ulaya (EU) kama ruzuku kwa wakulima wa chai wa Wilaya ya Rungwe mkoani hapa ili kuboresha kilimo cha zao hilo.

Fedha hizo zimetolewa kwa wakulima hao kupitia mradi wa kuboresha kilimo cha chai nchini unaotekelezwa na Shirika la IDH Tanzania kwa kipindi cha miaka minne.

Meneja wa mradi huo, Elikinda Tenga, alisema fedha hizo zitasaidia kuinua kipato na lishe kwa wakulima hao na kukabiliana na udumavu.

"Fedha hizi pia zitatumika kuwawezesha kuanzisha miradi midogo ya kuwaongezea kipato," alisema Tenga.

Alisema mbali na kilimo cha chai, wakulima hao watawezeshwa kuanzisha kilimo cha mazao ya bustani za mboga na matunda.

Akizungumza kwenye hafla ya kuwapongeza wakulima wa chai kwa kuhitimu mafunzo maalum ya kilimo bora cha chai, Mkuu wa Wilaya hiyo, Jafar Haniu, alisema fedha hizo zilitolewa kwa vyama vinane vya ushirika vya wakulima wa zao hilo.

**Fedha hizo zimetolewa kwa wakulima hao kupitia mradi wa kuboresha kilimo cha chai nchini unaotekelezwa na Shirika la IDH Tanzania kwa kipindi cha miaka minne.**

Katika hotuba yake iliyosomwa na Ofisa Kilimo wa Wilaya hiyo, Stephen Mbiza, alisema kuna wakulima zaidi ya 10,000 Rungwe ambao wamenufaika na fedha hizo.

Alisema fedha hizo zimetumika kununua vifaa kwa ajili ya kuwasaidia kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zinawakabili.

Mbiza, alisema vyama hivyo vilitumia fedha hizo kununua mitambo ya kuvuna chai, magari ya kukusanya zao hilo kutoka mashambani na kuanzisha miradi ya maendeleo yenye lengo la kuwasaidia wakulima kuondokana na kero ndogondogo zinazowakabili.

Baadhi ya wakulima, walisema mradi huo umewasaidia kuongeza uzalishaji.

Waliomba serikali kupandisha bei ya zao hilo ili ziendane na gharama za uzalishaji na kuwanusuru na hasara.



Kamishna wa Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dk. Charles Mwamwaja (kushoto), akimkabidhi zawadi mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Iyunga, jijini Mbeya aliyeibuka mshindi kwenye mashindano ya kuandika insha wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha ambayo yalihitimishwa mwishoni mwa wiki jijini hapa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mtaka: Mikopo umiza fedheha

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa Njombe, Anthony Mtaka ameziagiza taasisi za fedha mkoani hapa kutoa elimu kwa wafanyabiashara ili waachane na mikopo umiza mitaani na kuondokana na fedheha kwa kushindwa kurejesha kwa wakati.

Mtaka alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa uzinduzi wa huduma ya akaunti ya biashara kutoka Benki ya CRDB na mafunzo maalum kwa wafanyabiashara yaliyofanyika mjini hapa.

Alisema elimu hiyo itasaidia kufahamu mikopo yenye tija na kuachana na umiza ambayo imekuwa ikisababisha hasara katika biashara zao na fedheha kwa jamii wakati wa kunyang'anywa mali kama fidia ya mkopo kwa wanaoshindwa kulipa.

"Mtu anakuja na karatasi anakopa shilingi milioni moja halafu anarudisha milioni moja na laki saba na baada ya miezi mitatu anaambiwa wewe unadaiwa milioni tatu kumbe alikopa milioni moja, wameshauza makochi sasa waelimisheni kwamba huna haja ya kwenda kukopa mitaani mkadhalilika," alisema Mtaka.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Deo Sanga, aliziomba taasisi hizo kuharakisha kutoa mikopo kwa wafanyabiashara ili kuepuka kujiingiza kwenye taasisi za mitaani.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Halmashauri ya Mji Njombe, Eliud Pangamawe, alisema kuna tatizo la baadhi ya wafanyabiashara kukimbilia mikopo umiza kutokana na kushindwa kuhimili vigezo vigumu vinavyotolewa na taasisi za fedha nchini.

"Mikopo umiza ni rahisi mtu kuchukua kwa sababu masharti yake sio makubwa kama ya taasisi za fedha, mchakato hadi upate mkopo," alisema Pangamawe. Meneja wa Biashara wa benki hiyo Nyanda za Juu Kusini, Domina Mwita, alisema kuzinduliwa kwa akaunti hiyo mkoani hapa ni mkombozi kwa wafanyabiashara kutokana na mkoa kuwa na fursa nyingi za biashara.

"Tutahakikisha mikopo ya wafanyabiashara hawa ambao wameweza kuchangia katika benki kwa muda wa miaka mitatu shilingi milioni 75 inakwenda kutoka kwa wakati na kupata fursa wafanyabiasha wengine kutoka Mkoa wa Njombe," alisema Mwita.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Neema Kidugu, alitoa rai kwa wenzane kuhifadhi fedha benki na kuwa na sifa ya kukopesheka na kuachana na kukopa kiholela mitaani..

# TPA yaendelea kusaka wawekezaji

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetumia maonesho ya Tamasha la Biashara na Utalii Kusini kuendelea kunadi fursa za uwekezaji katika bandari zake nchini ili kuliongezea taifa mapato.

Maonesho hayo yanayofanyika wilayani hapa Mkoa wa Mbeya yalifunguliwa na Spika wa Bunge na Rais wa Mabunge Duniani, Dk. Tulia Ackson katika ufukwe wa Matema ulioko Ziwa Nyasa.

Akizungumza wakati wa maonesho hayo, Ofisa Uhusiano wa TPA, Leonard Magomba, alisema ni fursa muhimu ya kunadi maeneo ya uwekezaji katika bandari nchini na kuelezea wadau maboresho ya miundombinu yanayoendelea na yaliyokwisha kufanyika.

"Sote ni mashahidi wa faida za ushirikiano kati ya TPA na wawekezaji katika bandari zetu. Ufanisi umeongezeka sana husan katika Bandari ya Dar es Salaam tunashirikiana vyema na wabia wetu, ambao ni Kampuni za DP World na Tanzania East Africa Gateway Terminal Ltd," alisema Magomba.

Alisema tangu kuanza kwa wabia, ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam umeongezeka kwa kiwango kikubwa na kuvuka lengo la kuhudumia shehena ya tani milioni 27 kabla ya kufikia mwaka 2028.

Alisema TPA iliweka lengo la kuhudumia kiwango hicho cha shehena ifikapo mwaka 2027, miaka mitatu kabla limefikiwa.

Alisema uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kupitia TPA katika Bandari ya Dar es Salaam umetoa fursa za uwekezaji katika bandari hiyo ambayo kwa sasa inafanya kazi kwa mafanikio makubwa na wabia wake.

Alisema TPA pia imefanya maboresho katika Bandari ya Tanga kwa kuongeza kina na magati yake, ya Mtwara ikijengwa gati mpya namba 2 lenye urefu wa mita 300.

Kuhusu bandari za maziwa, alisema serikali inaboresha miundombinu katika Bandari za Mwanza Kaskazini, Kemondo na Bukoba upande wa Ziwa Victoria.

Magomba, alisema kwa Ziwa Nyasa, inajenga bandari mpya ya Mbambabay, Ziwa Tanganyika ya Karema, Kabwe, Ujiji na Kibirizi.

Kwa mwaka huu tamasha hilo limeshirikisha taasisi za serikali, umma, binafsi na wafanyabiashara wadogo wa ndani na nje ya nchi.



## Rais Mwinyi awapa nafuu wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezitaka taasisi za kusimamia masoko mapya kuweka viwango vidogo vya malipo ili wafanyabiashara na wajasiriamali wamudu gharama na kuendesha shughuli zao katika mazingira bora.

Rais Dk. Mwinyi alitoa rai hiyo jana wakati akifungua soko jipya la kisasa la Jumbi lililoko Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ikiwa ni mwendelezo wa shamrashamra za miaka minne ya uongozi wake.

Aliwahakikishia wafanyabiashara kuwa serikali itaendelea kuwaandalia mazingira bora zaidi sokoni hapo.

Alisema serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuwapatia mitaji wajasiriamali na wafanyabiashara ili kuimarisha biashara zao.

Dk. Mwinyi, aliwataka wajasiriamali ambao bado hawajapata mitaji kujiunga katika vikundi ili serikali iwapatie mitaji hiyo.

Alisema ni vyema masoko hayo ya kisasa aliyoyafungua yakafanya kazi kwa saa 24 na kuahidi wananchi kuendelea kutimiza ahadi zake za wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2020.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, alisema wakati wanaingia madarakani wapo waliodhani Dk. Mwinyi na serikali yake hawatafanya jambo lolote, lakini kwa sasa wanaona mambo makubwa zaidi ya malengo yao.

Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Masoud Ali Mohammed, alimpongeza Rais Mwinyi kwa kujenga mradi huo kwa maslahi kwa wananchi wa visiwani hapa.

Masoud alimhakikishia Rais Mwinyi wataendelea kuishi katika maono yake ili maendeleo ya wananchi anayoyatekeleza kupitia sekta mbalimbali yaweze kukamilika.

Akitoa maelezo ya ujenzi wa soko hilo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Issa Mahfoudh Haji, alisema ujenzi ulianza Februari Novemba 16 mwaka 2022 na kukamilika Oktoba 18, mwaka huu.

Alisema hadi ujenzi wa soko hilo lenye uwezo wa kichukua wafanyabiashara 4,000 unakamilika, umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 24.

# Mamilioni kusakwa vita dhidi ya udhalilishaji watoto, wanawake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

**Aliitaka jamii kuitikia wito huo kwa kuchangia fedha ili kufanikisha kampeni hiyo.**

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Taasisi ya "Ndoto Ajira ya jijini Dar es Salaam imeandaa kampeni ya kitaifa kwa lengo la kukusanya zaidi ya Sh. milioni 650 kwa ajili ya kupinga udhalilishaji watoto na wanawake visiwani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Waziri wa Wizara hiyo Riziki Pembe Juma, alisema kuwa kampeni hiyo yenye jina la Mtoto Mboni Yangu, itaendeshwa katika mikoa mitano vya Kisiwa cha Unguja na Pemba.

Riziki, alisema lengo la kampeni hiyo ni kukusanya fedha hizo kwa ajili ya kuzunguka Zanzibar kuelimisha wananchi jinsi ya kupinga vitendo hivyo katika jamii.

Riziki, alisema mwisho wa kampeni hiyo ya miezi mitatu itakuwa Desemba 30, mwaka huu.

"Kampeni hii imekuja ikiwa na azma ya kuunga mkono juhudi za Rais wetu wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kupinga ukatilii kwa wanawake na watoto," alisema.

Aliitaka jamii kuitikia wito huo kwa kuchangia fedha ili kufanikisha kampeni hiyo.

"Kwa pamoja tukishirikiana tunaweza kulitokomeza janga hili ndani ya nchi na Taifa letu ili kuwa na kizazi chenye maadili mema, " alisema waziri huyo.

Kaimu Mwenyekiti wa Kampeni hiyo, Edward Musimo, alisema lengo ni kutoa elimu kwa jamii juu athari ya vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto visiwani hapa baada ya kubaini ndio wahanga wakubwa.




Baadhi ya wafanyakazi wa Wilaya ya Magharibi "B" Unguja na wafanyabiashara wa Soko la Jumbi wakishangilia wakati Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), akihutubia katika hafla ya ufunguzi wa soko jipya la Jumbi juzi. **PICHA: IKULU**

# Wageni wanaoingia Z'bar wapungua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDADI ya wageni wanaoingia visiwani hapa kwa Septemba mwaka huu imepungua hadi kufikia 60,731.

Hayo yamo katika takwimu za uingiaji wageni visiwani hapa zilizowasilishwa jana kwa waandishi wa habari katika Ofisi za Mtakwimu Mkuu wa Serikali Mazizini.

Akiwasilisha takwimu hizo, Ofisa Tafiti na Takwimu, Hassan Ameir Vuai, alisema idadi hiyo ya wageni hao walioingia visiwani hapa kwa kipindi hicho ni ndogo kwa asilimia 16.0 ikilinganishwa na wageni 72,296 walioingia kwa Agosti mwaka huu.

Vuai, alisema takwimu hizo zinaonyesha kuna ongezeko la asilimia 12.8 la wageni walioingia nchini kwa Septemba, 2024 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka jana.

Alisema kipindi kama hicho kwa mwaka jana, wageni 53,839 walioingia visiwani hapa. Akizungumzia zaidi alisema kati ya wageni 60,731 kwa Septemba, mwaka huu, 42,589 ni kutoka Bara la Ulaya ambao ni sawa na asilimia 70.1 ya wageni wote.

Alisema kundi hilo ndilo linaloongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wageni wengi zaidi walioingia visiwani hapa kwa kipindi hicho cha mwezi mmoja.

Mtafiti huyo, alisema Bara la Afrika lilifuatia kwa kuwa na 8,352 sawa na asilimia 13.8 ya wageni wote.

Bara la Asia lilikuwa la tatu kwa kuwa na wageni 4,903 sawa na asilimia 8.1 na Oceania la mwisho kwa kuingiza wageni 681 sawa na asilimia 1.1 ya wageni wote.

Hata hivyo, alisema Italia iliongoza kwa kuleta wageni 7,511 sawa na asimilia 12.4 ya wageni wote ikifuatiwa na Ujerumani 6,728 (11.1), huku Ufaransa ikiwa ya tatu kwa kuwa na wageni 5,262 (8.7), Poland ya nne wageni 4,508 (7.4) na tano Uingereza 4,361 (7.2).

Alisema wageni hao waliingia Zanzibar kupitia viwanja vya ndege na bandarini.

Ofisa Takwimu na Utafiti Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Mabadi Jafar Mwadini, alisema Ulaya imeleta wageni wengi kutokana na matangazo mengi kuelekeza katika bara hilo.

Meneja wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Shirika la Bima Zanzibar, Bakar Mussa Yussuf, alisema licha ya kujitokeza changamoto nyingi kwa uanzishwaji bima kwa wageni, wengi wanaoingia visiwani hapa wanakataa bima.

Ofisa Uhusiano Idara ya Uhamiaji Zanzibar, Sharif Bakari Sharif, alisema kuwa bado kuna changamoto kwa baadhi ya wageni kuingia Zanzibar kupita katika bandari bubu.

VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa Tarehe 30/09/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/06/2024 |
|---|---|---|
| | TZS | TZS |
| **A. MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 212 | 99 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | – | – |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | – | – |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 14,279 | 9,778 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushungulikiwa | – | – |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | – | – |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | – | – |
| 8 Dhima ya Wateja Zilizokubalika | – | – |
| 9 Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | – | – |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | – | – |
| 11 | – | – |
| Mikopo Halisi Iliyopo | 45,932 | 45,517 |
| 12 Mali Nyingine | 4,144 | 3,180 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | – | – |
| 14 Akaunti za udhamini | – | – |
| 15 Mali Zisizohamishika ,Mitambo na Vifaa | 2,579 | 2,516 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **67,146** | **61,090** |
| | – | – |
| **B. DHIMA** | – | – |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | – | – |
| 18 Amana za Wateja | 5,178 | 5,882 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | – | – |
| 20 Amana Maalumu | 3,159 | 2,459 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | – | – |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | – | – |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 9 | 10 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | – | – |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | – | – |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 77 | 77 |
| 27 Zitakazolipwa Baadae | 5,722 | 3,875 |
| 28 Dhima Nyingine | 26,520 | 22,508 |
| **29 Madeni** | **40,665** | **34,811** |
| **JUMLA YA DHIMA** | **-** | **-** |
| **30 MALI/(DHIMA)HALISI (16 kutoka 29)** | **26,481** | **26,280** |
| | – | – |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | – | – |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,200 | 21,200 |
| 32 Akiba ya Mtaji | 2,796 | 2,737 |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | (2,119) | (2,119) |
| 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,337 | 863 |
| 35 Akauti Nyingine za Mtaji | 3,266 | 3,599 |
| **36 Stahiki ya Wenyehisa Chache** | – | – |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISANI** | **26,481** | **26,280** |
| | – | – |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | – | – |
| 39 Mikopo Chechefu | **1,384** | **1,475** |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | **1,106** | **1,005** |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | – | – |
| | – | – |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | – | – |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | **39%** | **43%** |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | **3.0%** | **3.2%** |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **561%** | **555%** |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **70%** | **76%** |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **81%** | **84%** |
| (vi) Ongezeko la Amana | **0.0%** | **3.0%** |
| (vii) Ongezeko la Mali | **9.9%** | **0.7%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024 (Kiasi kwa shilingi)

| | Robo ya Mwaka sasa 30/09/2024 | Robo ya Mwaka Linganishi 30/09/2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2023 |
|---|---|---|---|---|
| | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 Mapato ya Riba | 5,517 | 4,355 | 16,239 | 12,222 |
| 2 Gharama za Riba | 1,140 | 428 | 3,274 | 1,053 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **4,377** | **3,927** | **12,965** | **11,169** |
| | - | - | - | - |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (421) | **(253)** | (725) | **(560)** |
| | - | - | - | - |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,672** | **1,254** | **4,791** | **3,238** |
| | - | - | - | - |
| 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 149 | 71 | 295 | 276 |
| 6.2 Ada za Kamisheni | 978 | 771 | 3,202 | 2,162 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 545 | 412 | 1,294 | 801 |
| | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo na Riba :** | **4,812** | **4,744** | **15,352** | **12,667** |
| | - | - | - | - |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 2,422 | 2,195 | 7,493 | 6,315 |
| 7.2 Gharama Nyingine | 2,390 | 2,548 | 7,859 | 6,351 |
| 7.3 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | - | - | - | - |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **816** | **184** | **1,679** | **1,180** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 342 | - | 342 | - |
| **10 Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **474** | **184** | **1,337** | **1,180** |
| | 0 | - | - | - |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | **460** | **438** | **460** | **438** |
| 12 Mapato kwa Hisa | 22,358 | 8,692 | 63,062 | 55,684 |
| 13 Kipato kwa Hisa | 22,358 | 8,692 | 63,062 | 55,684 |
| 14 Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 Vituo Vya Biashara | 35 | 35 | 35 | 35 |
| 16 Vituo Vidogo | 12 | 12 | 12 | 12 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | - | - | - |
| (i) Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | 0.7% | 0.4% | 2.1% | 2.5% |
| (ii) Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.8% | 0.8% | 5.1% | 5.0% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 80% | 92% | 86% | 88% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalisha | **16%** | **20%** | **49%** | **57%** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma(Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 15 Oktoba 2024 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha) | | 15 Oktoba 2024 |
| Albert Chikira (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 15 Oktoba 2024 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1 Athanasia Soka ( Mwenyekiti ya Bodi) | | 15 Oktoba 2024 |
| 2 Jeff Mckrae (Mwendeshaji) | | 15 Oktoba 2024 |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/09/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/06/2024 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2023 |
|---|---|---|---|---|
| | TZS | TZS | TZS | TZS |
| **I: MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| Mapato/(Hasara)Hakisi | **474** | **337** | **1,337** | **1,180** |
| | - | - | - | - |
| **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| Hasara Katika Mali | 152 | 125 | 438 | 394 |
| Badiliko Halisi Katika Mikopo | (415) | (2,145) | (5,065) | (9,149) |
| Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Amana | (4) | 243 | 832 | 549 |
| Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (965) | (451) | (976) | (552) |
| Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| Mengineyo | 1,846 | (1,067) | 1,803 | 375 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| **kwa shughuli za uendeshaji** | **1,089** | **(2,958)** | **(1,631)** | **(7,202)** |
| | - | - | - | - |
| **II: MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | - | - | - | - |
| Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (215) | (66) | (1,009) | (920) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| **kwa Shughuli za uekezaji** | **(215)** | (66) | (1,009) | (920) |
| | - | - | - | - |
| **III: MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **4,012** | - | 3,995 | 10,010 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 59 | 913 | 1,259 | 1,146 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo | (332) | 9 | (745) | 283 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| **kwa Shughuli za Kifedha** | **3,739** | **922** | **4,509** | **11,440** |
| | - | - | - | - |
| **IV: FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | - | - | - | - |
| Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tastimu | 4,614 | (2,102) | 1,869 | 3,318 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 9,878 | 11,980 | 12,622 | 5,569 |
| | - | - | - | - |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu /** | - | - | - | - |
| **Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **14,491** | **9,878** | **14,491** | **8,887** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2024 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2024)** | **21,200** | **(1,646)** | **0** | **5,076** | **24,630** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | **-** | **1,337** | **-** | **-** | **1,337** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | **2,796** | **(473)** | **-** | **(1,810)** | **514** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **23,996** | **(782)** | **0** | **3,266** | **26,481** |
| | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2023)** | **21,200** | **(2,418)** | **0** | **2,292** | **21,074** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | **-** | **755** | **-** | **-** | **755** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | **-** | **17** | **-** | **2,784** | **2,801** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **(1,646)** | **0** | **5,076** | **24,630** |

## ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA

| Huduma za Kibenki | | | Gharama-(Pamoja na VAT) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuangalia Salio-Dirishani & ATM | | 554 |
| 2 | Kuhamisha fedha | Ndani ya VFT hadi TZS1,000,000 | 944 |
| | | Ndani ya VFT zaidi ya TZS1,000,000 | 1,180 |
| | | Kwenda Benki nyingine hadi TZS10,000,000 | 3,554 |
| | | Kwenda Benki Nyingine zaidi ya TZS10,000,000 | 11,800 |
| 3 | Kutoa disrishani hadi/Kwakila TZS 5,000,000 | | 1,770 |
| 4 | Kutoa ATM | | 1,500 |
| 5 | Kadi ya ATM (Mpya au Kubadili) | | 5,000 |
| 6 | Gharama za mwezi (Monthly Acc maintanance fees) | Akiba Akaunti | 885 |
| | | Akaunti ya Biashara | 1,770 |
| 7 | Kufunga Akaunti | Akaunti ya Akiba, Watoto & Dunduliza | 2,360 |
| | | Akaunti ya Vikundi na Biashara | 5,900 |
| 8 | Taarifa ya Akaunti | Taarifa Fupi ATM | 720 |
| | | Miezi 0-1 | Bure |
| | | Miezi 1-3 | 1,180 |
| | | Miezi 3-12 | 3,540 |
| | | Miezi 12-24 | 11,800 |
| | | Miezi 24-48 | 29,500 |
| | | Miaka 3-6 | 41,300 |
| | | Zaidi ya miaka 6 | 55,400 |

| Huduma Za Simu (Mobile banking) | | | | Gharama-(Pamoja na VAT) |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Kujua Salio-Simu | | | 118 |
| 10 | Kutoa kwa simu-Kuanzia tarehe 1 Decemba 2024 | Kiwango cha chini | Kiwango cha juu | |
| | | Chini ya 100,000 | | 1,180 |
| | | 100,000 | 199,999 | 1,770 |
| | | 200,000 | 299,999 | 2,360 |
| | | 300,000 | 399,999 | 2,950 |
| | | 400,000 | 499,999 | 3,540 |
| | | 500,000 | 1,000,000 | 4,720 |
| 11 | Kuhamisha Fedha-Simu | | | 118 |
| 12 | Taarifa Fupi-Simu | | | 354 |
| 13 | Kubadili Number ya Siri | | | 236 |

**Akaunti**

| s/n | Huduma | Kiwango cha chini | Riba Kwa mwaka * |
|---|---|---|---|
| 1 | Akiba Akaunti | 5,000 | 3% |
| 2 | Salary Akaunti | 5,000 | 3% |
| 3 | Kikundi Akaunti | 20,000 | 4% |
| 4 | Watoto Akaunti | 10,000 | 4% |
| 5 | Biashara Akaunti | 100,000 | 3% |
| 6 | Fixed Deposit Accounts | N/A | Kulingana na muda na Kiasi |
| 7 | Dunduliza Akaunti | 10,000 | 4% |

** Riba kwa akaunti za aina zote itajilimbikiza kwa kila la siku kwa kiasi cha akiba cha TZS100,000 na kuendelea na kulipwa kila Mwezi.*

**Mikopo ya Vikundi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mikopo ya Vikundi -Biashara group Loan | 5% | 60% | 3% | 1% |
| 2 | Mikopo ya Vikundi/Savings Group Loan | 5% | 60% | 2.5% | 0% |
| 3 | Mikopo ya Vikundi -Jiendeleze Group Loan | 4% | 48% | 3.1% | 1% |

**Mikopo Binafsi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Mkopo Binafsi Na shule- hadi TZS10M | 4% | 48% | 2.5% | 1% |
| 5 | Mkopo Binafsi na shule inayozidi TZS10M Hadi TZS 20M | 3.50% | 42% | 2.5% | 1% |
| 6 | Mikopo Binafsi na shuke inayozidi TZS20M | 2.50% | 30% | 2.5% | 1% |
| 7 | Elimisha | 4% | 48% | 3.5% | 1% |

**Mikopo ya Kilimo**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | Mikopo Binafsi -Jikomboe Loan | 4% | 48% | 4.0% | 1% |
| 10 | Mikopo ya kikundi -Jitume | 5% | 60% | 4.0% | 1% |
| 11 | Mikopo ya Kikundi -Mkombozi Loan | 5% | 60% | 4.0% | 1% |
| 12 | Patnerships | 3% | 36% | 3% | 1% |

| | | |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma(Ofisa Mtendaji Mkuu) | Sahihi | 15 Oktoba 2024 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha) | Sahihi | 15 Oktoba 2024 |
| Albert Chikira (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | Sahihi | 15 Oktoba 2024 |

# WAZIRI MKUU: WATANZANIA TUULINDE UTAMADUNI WETU

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kuhakikisha wanalinda utamaduni na kujenga misingi ya kuhamasisha vijana na vizazi vijavyo kutambua na kuenzi historia na urithi wa Mtanzania.

**Majaliwa alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akifungua Tamasha la Buhaya 2024 'Buhaya Festival' lililofanyika Mlimani City, jijini Dar es Salaam.**

Alisema ni wajibu wa kila Mtanzania kutunza utamaduni, mila na desturi kwa sababu ni nguzo ya utambulisho wa jamii husika na ni muhimu kwa kizazi kijacho.

"Katika siku za sasa, ambapo teknolojia na utandawazi vinazidi kuimarika, ni rahisi kupoteza mila na desturi zetu, hivyo tunaposhiriki tamasha hili, tunajifunza na kuhamasisha jamii zetu kuhusu umuhimu wa urithi wetu wa kiutamaduni," alisema.

Kadhalika, Majaliwa amewaasa wazazi, jamii na madhehebu ya dini kuendelea kuhimiza utunzaji wa maadili kwa kuzingatia mila na desturi ili kuepuka mmomonyoko wa maadili kwa vijana na jamii kwa ujumla.

"Watanzania wote tuendelee kuheshimu na kuenzi tamaduni zilizo nzuri kama njia ya kuimarisha umoja, mshikamano na maendeleo ya kiuchumi," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Majaliwa ameiagiza mikoa yote nchini kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi kuweka mipango ya kuandaa matamasha ya utamaduni kuanzia ngazi za wilaya ili kuendeleza na kuhifadhi vivutio, mila na desturi za maeneo husika.

Akizungumzia kuhusu maendeleo ya Mkoa wa Kagera, alisema kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika mkoa huo kwenye sekta za nishati, maji, kilimo, uvuvi, uchukuzi na ujenzi wa barabara.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa, alisema tamasha hilo linalowaleta pamoja Wanakagera, linalenga kulinda na kutangaza utamaduni, mila na desturi za Wanakagera pamoja na kutangaza vivutio na fursa zilizoko mkoa wa Kagera.

"Buhaya inaendelea kukumbukwa kwa maadili, ushirikiano na ujasiri uliojengwa na wazee wetu, pia kupitia tamasha hili mkoa umetangazwa sana, mila na desturi zimeenziwa."

Naye Mwenyekiti wa Tamasha hilo, Wilson Kazaura, alisema tamasha hilo ni zaidi ya burudani kwani linatoa fursa kwa jamii ya Wahaya kuungana, kujifunza na kuhifadhi urithi wa kitamaduni kwa vizazi vijavyo.

"Tutaendelea kushikamana na serikali katika kuenzi tamaduni ili tuweze kurithisha kwa vizazi vijavyo na tutaendelea kuenzi sanaa, mila na desturi ambazo ni utambulisho wetu".

## MBAYA WA TEN HAG...



Winga wa West Ham United, Jarrod Bowen (juu), akishangilia baada ya kufunga bao la pili na la ushindi kwa mkwaju wa penalti dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa London juzi na West Ham kushinda 2-1. Kipigo hicho kimeufanya uongozi wa Man United kumtimua Kocha Erik ten Hag kutokana na mfululizo wa matokeo mabaya. **PICHA: MTANDAO**

# Mbeya Kwanza, Cosmopolitan zatakata Ligi ya Championship

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 1968, Cosmopolitan na Mbeya Kwanza iliyoshuka daraja msimu wa 2021/22, juzi zilipata ushindi kwenye Ligi ya Championship, katika harakati za kutaka kupanda kwa daraja msimu wa 2025/26.

Ikiwa ugenini, Uwanja wa Jamhuri Morogoro, Cosmopolitan iliitandika Kiluvya FC mabao 3-1 na kuifanya kusogea kidogo juu, ikipanda hadi nafasi ya 11 ya msimamo ikiwa na pointi saba.

Kiluvya, ambayo ilipanda msimu huu kutoka 'First League', bado inaendelea kukamata mkia kwenye ligi hiyo, ikiwa imepoteza michezo yote sita iliyocheza mpaka sasa.

Kwingineko kwenye Uwanja wa Kambarage, Shinyanga, wenyeji Stand United walipoteza mechi nyumbani kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya kwanza.

Bao pekee kwenye mchezo huo lilifungwa na Seifa Adam Selemani katika dakika ya 69 ya mchezo na kusimama hadi dakika 90 za mchezo.

Ushindi huo unaifanya Mbeya Kwanza kupaa hadi nafasi ya saba ya msimamo ikiwa na pointi 10, na kuizuia Stand United kupanda juu, ikibakia kwenye nafasi ya nne na pointi zake 12.

Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Emmanuel Massawe, amewapongeza vijana wake kwa kupambana hadi kupata ushindi huo akisema si rahisi kuifunga Stand United ikiwa nyumbani kwao.

"Ni ushindi wa kujivunia, Stand United ni moja kati ya timu ngumu kwenye ligi hii, hata msimamo unaonesha hivyo, kwa hiyo tunapaswa kujivunia," alisema.

Kocha Mkuu wa Stand United, Meja Mstaafu, Abdul Mingange, amekiri kupoteza akisema wachezaji wake hawakutumia vema nafasi, lakini akiangalia zaidi mchezo ujao.

"Mchezo umeisha, hata tuseme vipi hatuwezi kubadilisha, nitakwenda kurekebisha pale ambapo naona kuna mapungufu," alisema.

# Taifa Stars yaahidi kuwaliza Sudan kwa Mkapa

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Sudan katika mchezo wa hatua za mtoano kwa ajili ya kusaka nafasi ya kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, imeahidi kulipiza kisasi katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Jumapili, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza kutoka nchini Mauritania ambako mchezo huo ulipigwa juzi usiku, kwenye Uwanja wa de la Capitale, jijini Nouakchott, nahodha wa timu hiyo, Aishi Manula, alisema ana uhakika watafanya vema katika mchezo wa marudiano kutokana na jinsi wachezaji wenzake ambao wengi bado ni vijana walivyopambana katika mchezo huo licha ya kwamba wengi wao walikuwa wanacheza kwa mara ya kwanza.

Sudan inacheza mechi zake nchini humo kutokana na kuwapo kwa machafuko na vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini kwao.

"Tumemaliza mchezo wetu salama salimini, kazi kubwa imefanyika, pamoja na kupoteza lakini wachezaji hawa vijana wamepambana sana ugenini. Muda ulikuwa ni mfupi sana wa maandalizi na wachezaji wengi ni chipukizi, wengine ni mara ya kwanza kucheza Stars, walionekana kuwa na presha kubwa mwanzoni, lakini baadaye wakaonesha uwezo mkubwa," alisema Manula.

Alisema kwa sasa wana muda mrefu wa kukaa kambini na kumpa uwanja mpana Kocha Mkuu, Bakari Shime, kuendelea kukisuka kikosi na kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kwenye mchezo uliopita.

"Kikubwa tunakwenda nyumbani, tuna muda mrefu sasa wa kujiandaa kwa sababu hatuvunji kambi, mwalimu ana nafasi kubwa ya kusahihisha kile ambacho anaona kimekosewa katika mchezo wa kwanza, nadhani katika uwanja wa nyumbani tutafanya vizuri zaidi kuliko leo," alisema.

Juzi, Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), lilitangaza kuwa mchezo huo wa marudiano utapigwa saa 10:00 jioni, Uwanja wa Benjamin Mkapa na hakutakuwa na kiingilio.

## ZISIKUPITE

### ALEXANDER-ARNOLD ASAKWA

KLABU ya Paris St-Germain imeungana na Real Madrid katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa kulia wa Liverpool mwingereza Trent Alexander-Arnold, 26. ***(Mail)***

### DEDIC ANYATIWA LIVER

LIVERPOOL wameulizia kuhusu beki wa kulia wa RB Salzburg raia wa Bosnia na Herzegovina, Amar Dedic, ambaye anatarajiwa kuchukua nafasi ya Trent Alexander-Arnold. ***(Caught Offside)***

### CHAKBETADZE ALENGWA

WOLVES wamemfanya kiungo mkabaji wa Watford na Georgia, Giorgi Chakvetadze mwenye miaka 25, kuwa mchezaji wanayemlenga Januari. ***(Sun)***

### ALONSO ATAKIWA MADRID

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez, anaandaa misingi ya nani atakayechukua nafasi ya kocha, Carlo Ancelotti, msimu ujao huku akimpigia debe Kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso. ***(Sport)***

### BALOTELLI ATUA GENOA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Italia, Mario Balotelli mwenye miaka 34, amefanyiwa vipimo vya matibabu siku ya jana kabla ya kusajiliwa na Klabu ya Serie A, Genoa. ***(Fabrizio Romano)***

### WEST HAM KWA LOOKMAN

KLABU ya West Ham inavutiwa na mshambuliaji wa Atalanta na Nigeria, Ademola Lookman mwenye umri wa miaka 27, wakati huu kocha Julen Lopetegui akitumai kuimarisha safu yake ya mashambulizi Januari. ***(GiveMeSport)***

### GVARDIOL KUONGEZEWA

KLABU ya Manchester City inajiandaa kumpa mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol mwenye miaka 22, mkataba ulioboreshwa wenye thamani ya pauni 150,000 kwa wiki ili kuongeza muda wake wa kukaa Etihad hadi 2030. ***(Star)***

### PALMER KUBAKI CHELSEA

KIUNGO mshambuliaji wa England na Chelsea Cole, Palmer mwenye miaka 22, bado anajitolea kwa 'The Blues' hao licha ya kuhusishwa na kutaka kuondoka, ikiwa ni pamoja na kurejea Manchester City. ***(Football Insider)***


### CHIESA KUREJA ITALIA

AC Milan ina nia ya kumpa njia ya kurejea Serie A, winga wa Liverpool na Italia, Federico Chiesa, 27. ***(Caught Offside).***

### HUMMELS KUONDOKA

BEKI wa zamani wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35, anaweza kuondoka AS Roma Januari licha ya kujiunga na klabu hiyo ya Serie A kama mchezaji huru msimu wa majira ya joto. ***(Nicolo Schira)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: ARSENAL IKO HAI KWA MBIO ZA UBINGWA

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amepunguza umuhimu wa pengo la pointi tano kwa vinara wa Ligi Kuu England Manchester City kwa kusifia timu yake kuwa hai katika mbio za ubingwa baada ya sare ya mabao 2-2 na Liverpool Jumapili.

**Bukayo Saka alifunga bao la kuongoza likiwa lake la 50 la ligi baada ya dakika tisa kabla ya Virgin van Dijk kusawazisha kwa kichwa dakika ya 18.**

Mikel Merino alifunga kwa kichwa mpira wa adhabu wa Declan Rice na kurejesha uongozi wa 'Washikabunduki', kabla ya kipindi cha mapumziko, lakini bao la kusawazisha la Mohamed Salah la dakika ya 81 liliokoa pointi moja kwa Liverpool.

Liverpool wanasalia katika nafasi ya pili, pointi nne mbele ya Arsenal ambao wanashika nafasi ya tatu huku City wakifurahia kileleni wakati huu wakisaka taji la tano mfululizo.

> ●●● Wanaojeruhiwa, waliopo, wapo katika wakati mzuri, tunaenda kuwa mahali pazuri...

Alipoulizwa jinsi tofauti ya pointi katika hatua hiyo ya mwanzo ya msimu, Arteta alisema: "Hutaki kuwa katika nafasi hiyo. Unataka kuwa mbele kwa pointi tano, lakini hapa ndipo tulipo. Timu iko hai.

"Wanaojeruhiwa, waliopo, wapo katika wakati mzuri. Mambo yatatokea na tunaenda kuwa mahali pazuri zaidi.

"Naona timu na sina mashaka, nadhani nilikuambia siku tatu kabla kwamba tutapanda ndege Jumapili na tulianza kuruka na tulikuwa timu bora zaidi.

"Tulihitaji kupata pointi leo (juzi) ili kutafakari tulipo na tunapotaka kuwa. Hatukuweza kufanya hivyo lakini kwa uhakika tupo."

## HABARI MICHEZO



# TEN HAG ATIMULIWA UNITED, VAN NISTELROOY KUIONGOZA

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imemfuta kazi kocha, Erik ten Hag, baada ya kuiongoza klabu hiyo kwa muda wa miaka miwili na nusu.

Raia huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 54, alitaarifiwa kuhusu uamuzi huo na bodi ya klabu hiyo jana Jumatatu asubuhi.

Man United imeanza vibaya msimu huu huku mechi ya mwisho ya Ten Hag ikiwa ya juzi Jumapili ambapo walifungwa mabao 2-1 na West Ham kwenye Ligi Kuu England.

United pia ipo katika nafasi ya 21 kati ya timu 36 kwenye msimamo wa la Ligi ya Europa, wakiwa wametoka sare katika mechi zao tatu za mwanzo. Ruud van Nistelrooy, ambaye alijiunga na klabu hiyo kama kocha msaidizi wa Ten Hag msimu uliopita wa majira ya joto, ametajwa kuwa kocha wa muda hadi kocha mkuu wa kudumu atakapoajiriwa.

Klabu hiyo ilikuwa imeongeza mkataba wa Ten Hag kwa mwaka mmoja baada ya ushindi wa fainali ya Kombe la FA Mei mwaka huu walipoifunga Manchester City. United sasa wanatafuta kocha wao wa sita wa kudumu tangu Sir Alex Ferguson alipostaafu mwaka 2013.

Ten Hag ambaye ni kocha wa zamani wa Ajax alichukua mikoba ya kuinoa Man United msimu wa majira ya joto mwaka 2022 na kuiongoza klabu hiyo kushika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu katika msimu wake wa kwanza.

Pia, aliiongoza United kutwaa taji lao la kwanza katika misimu sita kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Newcastle United kwenye fainali ya Kombe la Carabao 2023.

Msimu wake wa pili kama kocha wa klabu hiyo ulianza vibaya, huku United wakimaliza mkiani katika kundi lao la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini wakatwaa Kombe la FA.

Kampuni ya Sir Jim Ratcliffe ya Ineos ilinunua asilimia 27.7 ya hisa za klabu hiyo mnamo Desemba 2023 na bilionea huyo wa England aliiambia BBC Sport Februari kuwa matatizo ya klabu hiyo yaliongezeka zaidi ya jukumu la kocha.

"Katika miaka 11 iliyopita, Manchester United imekuwa na makocha wengi na hakuna aliyefanikiwa katika nyanja hiyo," alisema Ratcliffe. "Hiyo kwangu inamaana kwamba kuna kitu ambacho hakiko sawa kimazingira."




# Van Dijk hana haraka na mkataba mpya

**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk amesema atasimamisha mazungumzo ya mustakabali wake na Liverpool hadi mwishoni mwa msimu huu.

Van Dijk, Salah na Trent Alexander-Arnold wote mikataba yao itamalizika Anfield mwishoni mwa msimu huu.

Akizungumza baada ya mchezo dhidi ya Arsenal uliochezwa Emirates juzi, Van Dijk alisema hana haraka ya kufanya mazungumzo ya kusaini mkataba mpya klabuni hapo.

"Nimetulia sana," alisema Van Dijk akiiambia Sky Sports.

"Wacha tuone nini kitatokea mwishoni mwa msimu.

"Ninafurahia soka langu, kimwili na kiakili. Naendelea kufurahia mchezo kwa sababu ni mchezo mzuri ambao tunacheza."

# Mashabiki wa Real Madrid wachunguzwa kwa ubaguzi

**MADRID,** Hispania

VINICIUS Junior amelaani matusi ya kibaguzi yaliyoelekezwa kwa wachezaji wa Barcelona na mashabiki wakati wa El Clasico kuwa "ya kutisha" baada ya LaLiga kusema kuwa inaripoti tukio hilo kwa polisi na waendesha mashtaka wa uhalifu wa chuki.

Picha za video zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii zilionekana kumwonesha Lamine Yamal akitukanwa alipokuwa akisherehekea na wachezaji wenzake baada ya kuifungia Barcelona bao la tatu katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Real Madrid Uwanja wa Santiago Bernabeu.

"Kilichotokea pale Bernabeu na matusi ya kibaguzi kilikuwa mbaya," Vinicius alichapisha kwenye X.

"Hakuna nafasi kwa wahalifu hawa katika jamii yetu.

"Msaada wangu wote kwa Lamine, Ansu Fati na Raphinha. Ninajua kwamba Madrid na polisi watachukua hatua kuwatambua na kuwaadhibu wahalifu!"

Hapo awali, LaLiga ilielezea unyanyasaji wa ubaguzi wa rangi kama "usiovumilika."

"LaLiga itaripoti mara moja matusi na ishara za kibaguzi zilizoelekezwa kwa wachezaji wa Barcelona kwa polisi, na pia kumjulisha mwendesha mashtaka anayeratibu uhalifu wa chuki na kitengo cha uhalifu wa ubaguzi katika ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali," taarifa ya LaLiga ilisema.

"LaLiga inalaani vikali matukio yaliyotokea Santiago Bernabeu na inabaki imara katika dhamira yake ya kutokomeza aina yoyote ya tabia ya ubaguzi wa rangi na chuki ndani na nje ya viwanja. Hakuna nafasi ya janga hili katika michezo."

Madrid pia ililaani unyanyasaji huo, ikisema uchunguzi unaendelea.

"Real Madrid inalaani vikali tabia yoyote inayohusisha ubaguzi wa rangi, chuki dhidi ya wageni au vurugu katika soka na michezo, na inajutia sana matusi yaliyofanywa na mashabiki wachache kwenye moja ya kona za uwanja," taarifa ya Madrid ilisema katika taarifa yake.

"Real Madrid imefungua uchunguzi ili kuwasaka na kuwabaini wahusika wa matusi haya ya kusikitisha na ya kudharauliwa, ili kuchukua hatua stahiki za kinidhamu na kimahakama."

# MECHI SIMBA, JKT YAAHIRISHWA

Na Adam Fungamwango

BODI ya Ligi nchini (TPLB), imeahirisha mchezo namba 79 kati ya Simba na JKT Tanzania uliokuwa uchezwe leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam kutokana na wachezaji, benchi la ufundi na baadhi ya viongozi wa timu hiyo ya jeshi kupata ajali juzi.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, amesema mchezo huo umeahirishwa baada ya uongozi wa JKT Tanzania kuwasilisha maombi rasmi ili kushughulikia hali ya wachezaji wao waliojeruhiwa.

Mbali na mchezaji huo, Bodi ya Ligi pia imeahirisha mchezo mwingine namba 89, ambao timu hiyo ilitakiwa kwenda kucheza dhidi ya Namungo, Novemba 4, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

JKT Tanzania ilipata ajali ilipokuwa inatoka jijini Dodoma kucheza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji uliopigwa, Uwanja wa Jamhuri, Jumamosi iliyopita na kufungwa bao 1-0

"Si kawaida, huwa mnaniona pembeni yangu kukiwa na makocha na manahodha, leo nipo peke yangu.

"Ni kwa sababu tumepokea taarifa kutoka Klabu ya JKT Tanzania kupata ajali hapo jana (juzi), wakiwa safarini kutoka Dodoma ambako walikuwa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Dodoma Jiji.

"Basi lililokuwa limebeba wachezaji, makocha na viongozi wengine lilipata ajali maeneo ya Mbweni, hivyo kwa niaba ya Bodi ya Ligi tunawapa pole sana, tukiwaombea wachezaji na viongozi wengine ambao wamepata maumivu wapate nafuu ya mapema na waendelee na mapambano katika msimu huu wa ligi," alisema Boimanda.

Alisema bada ya ajali hiyo waliwasiliana na viongozi wa JKT Tanzania, pamoja na Kamati ya Tiba ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), ambayo ilikwenda kuungana na matabibu wengine ili kuangalia afya za wachezaji.

"Baada ya ajali tuliwasiliana na viongozi wa JKT Tanzania, pamoja na Kamati ya Tiba ya Shirikisho la Mpira wa Miguu, ambapo Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Limbanga, alifika hospitalini ili kuangalia hali za wachezaji hao na kujiridhisha jinsi wanavyoendelea na baadhi yao jana walitarajia kupiga picha za X-ray, kwa ajili ya uchunguzi zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa JKT Tanzania, Jemedari Said, basi hilo lilipata ajali juzi saa 1:00 asubuhi eneo la Mbweni baada ya kuacha njia ya kutumbukia mtaroni.

Baadhi ya wachezaji waliojeruhiwa ni John Bocco, Danny Lyanga, Salum Gado, Gamba Matiko, Said Ndemla, Yacoub Suleiman, Hassan Dilunga, Maka Edward, Hassan Kapalata, Hassan Machezo na Mohamed Bakari.

# YANGA, JKCI ZAINGIA MKATABA KUSAIDIA MATIBABU YA MOYO

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Yanga na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), zimetia saini mkataba wa huduma za afya na elimu kwa umma kwa lengo la kupanua zaidi huduma hiyo na kuwafikia wagonjwa kwa urahisi.

Katika makubaliano hayo yaliyofanyika katika Hospitali ya Muhimbili jana, Klabu ya Yanga itanufaika kwa kupewa daktari na taasisi hiyo kila timu yake inapokwenda kucheza kwa ajili ya kupima wachezaji, lakini pia wanachama mashabiki watanufaika kwa kupimwa bure.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Mtine na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Dk. Peter Kisenge, walitia saini mkataba huo jana kila mmoja akiiwakilisha taasisi yake.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Dk. Kisenge, alisema kutakuwa na faida nyingi kwa pande zote mbili kutokana na makubaliano hayo, huku wao wakitaka watu mbalimbali Afrika kuifahamu taasisi hiyo.

"Kuungana na Yanga kutakuwa na faida nyingi, kwa kuitumia klabu hii, watu wengi wa Afrika wataifahamu taasisi yetu kwa sababu inapokwenda kucheza katika michezo mbalimbali ya kimataifa itakuwa inaieleza pia taasisi yetu, kwetu sisi tutakuwa tunawapa daktari wetu ambaye atakuwa anahudumia wachezaji kuwapima moyo na matatizo mengine, sisi tupo tayari kuwasindikiza kule mnapokwenda, hapa nchini na nje ya nchi," alisema Dk. Kisenge.

Alisema wanachama na mashabiki wa klabu hiyo pia watapata faida ya kupimwa ugonjwa huo bure na kupata ushauri nini cha kufanya kukabiliana na ugonjwa huo.

"Taasisi hii inawahudumia wagonjwa 900 kwa siku moja, ilianza 2015, tulianza tukiwa hapa, lakini sasa tuna tawi lingine Dar Group, wanachama na mashabiki wa Yanga nao watapata faida, kwani inawezekana kabisa kwenye matamasha kama ya Siku ya Mwananchi tukawapima bure," alisema.

Alisema kwa maana hiyo ushirikiano huo utakuwa na tija kwa pande zote mbili, kwani mbali na wachezaji kunufaika, kujulikana kwa taasisi hiyo barani Afrika ambako timu hiyo itakuwa inakwenda kucheza, hivyo kuwapata wananchi mbalimbali barani Afrika ambao wana uhitaji wa vipimo na matibabu ya ugonjwa huo.

Kwa upande wake, Mtine alishukuru taasisi hiyo ya Jakawa Kikwete kwa kurejesha kwa jamii, huku akisema familia ya michezo inatakiwa iwe na furaha wakati wote.

Aliiomba taasisi hiyo ikiwezekana wawe wanasafiri na jopo la matabibu wanapokwenda kucheza mechi mikoani, ambako watakuwa wakifanya kliniki ya kupima wananchi.

"Tunapokuwa tunasafiri nao kwenye michezo mbalimbali mikoani, wanaweza kuweka kliniki kwa ajili ya kupima si mashabiki na wanachama wa Yanga tu, bali wananchi pia wa mikoa hiyo na kuwapa ushauri, hivyo watakuwa wamepunguza kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa ugonjwa hatari kati ya magonjwa yasiyoambukiza," alisema.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Mtine (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikweye (JKCI), Dk. Peter Kisenge, wakionyesha jezi maalum baada ya kutia saini mkataba wa huduma za afya na elimu kwa umma kwa lengo la kupanua zaidi huduma hiyo na kuwafikia wagonjwa kwa urahisi. Hafla ya ya utiaji saini hiyo ilifanyika Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## *Mwamnyeto, Job wafichua siri ya ukuta 'jiwe' Yanga*

INATOKA UKURASA 24

mgumu zaidi kuliko walivyocheza dhidi ya Coastal Union, Jumamosi iliyopita kwani msimu huu imekuwa ni moja kati timu tishio.

"Mechi ya Jumatano (kesho), itakuwa ngumu, Singida ni timu nzuri na imesajili wachezaji wazuri sana msimu huu, lakini kwetu Yanga msimamo wetu ni ule ule, kukusanya pointi tatu kila mchezo, mastraika wetu watutafutie bao moja tu, sisi mabeki tutalinda, wakifunga mengine ni bonasi, tunachohitaji kila mchezo ni pointi tatu tu," alisema nahodha huyo.

Aliwataka mashabiki wa soka Zanzibar kujitokeza kwa wingi ili kuwapa burudani, lakini kuwapa furaha wanachama na mashabiki wa Yanga.

Kwa upande wa Job, alisema hawajaruhusu bao lolote mpaka sasa kutokana na mfumo ambao wamekuwa wakiutumia wa kurudi wengi nyuma kukaba badala ya kazi hiyo kuachiwa mabeki peke yao.

"Huwa tunacheza kwa mifumo mingi, lakini mara nyingi tunasaidiana majukumu, tunapokwenda kushambulia tunawasaidia kidogo, lakini tunaposhambuliwa siyo jukumu la mabeki peke yake, kukaba linakuwa ni jukumu la wachezaji wote kuanzia mastraika, viungo washambuliaji, wakabaji, ili kuturahisishia kazi sisi, na hilo limekuwa likitufanya mabeki tuwe na ufanisi kwenye kazi yetu," alisema beki hiyo.

## Fadlu: Ikifika Februari...

INATOKA UKURASA 24

osajiliwa msimu huu baada ya kuondoa rundo la wachezaji wengi wakongwe, imecheza michezo rasmi 10, minane ya Ligi Kuu na miwili ya kimataifa.

Katika michezo hiyo, imeshinda saba, sare mbili na kupoteza mmoja tu dhidi ya Yanga kwa bao 1-0, ambao ulipigwa Oktoba 19, mwaka huu.

Wakati inacheza michezo hiyo, Fadlu, amekuwa akisisitiza kuwa kikosi chake bado hakijawa sawa kimuunganiko, lakini akiwashangaza wengi kwani pamoja na upya na kukosa muunganiko kimekuwa na mabadiliko tofauti na cha misimu miwili iliyopita, ambapo mbali na kukonga nyoyo ya wanachama na mashabiki kutokana na kinavyocheza, lakini kimekuwa kikipata ushindi kwenye michezo mingi kinayocheza.

# Michezo


Jumanne Oktoba 29, 2024

Nipashe




## Arteta: Arsenal iko hai mbio za ubingwa

UKURASA 21




CHUMA HICHO...

Kiungo wa Arsenal, Mikel Merino (jezi namba 23), akiifungia timu yake kwa kuunganisha kwa kichwa mpira wa faulo uliopigwa na Declan Rice kwenye mechi kali ya Ligi Kuu England dhidi ya Liverpool iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# Fadlu: Ikifika Februari Simba haitokamatika

**Na Adam Fungamwango**

## Asema itatisha ndani na Afrika nzima na kila mtu ataiimba, mechi yao...

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, amesema ifikapo Februari mwakani, kikosi chake kitakuwa moto wa kuotea mbali si Tanzania tu bali hata kwenye michezo ya kimataifa barani Afrika, akiwataka wote wanaotoa maoni yao juu ya kikosi hicho kusubiri mpaka wakati huo.

**Akizungumza jijini Dar es Saaam jana, raia huyo wa Afrika Kusini, alisema licha ya kwamba tayari atakuwa ameshaongeza wachezaji kipindi cha usajili wa dirisha dogo, lakini kitaalamu, atakuwa ameshakinoa kikosi hicho kwa muda wa miezi sita huku kikiwa kinapambana uwanjani.**

"Kitaalamu ni kwamba klabu yoyote inaposajili kiasi cha wachezaji 15 na kocha mpya inatakiwa miezi sita ili kuona kiwango halisi cha timu na muunganiko wa wachezaji, kwani watakuwa wameshaelewana mikimbio, mifumo, sifa na udhaifu wa kila mchezaji ili kusaidiana uwanjani, tulianza ligi na michuano ya kimataifa Agosti, tukiwa na kikosi kichanga kinachojengwa, kipindi hiki tunamalizia ujenzi, lakini mabadiliko yanaonekana," alisema kocha huyo.

Alisema kwa michezo minane ya Ligi Kuu ambayo timu yake imecheza mpaka sasa, na miwili ya Kombe la Shirikisho, inaonekana inapiga hatua, lakini bado mpaka Februari mwakani ndipo kikosi hicho kitakuwa kimeshakamilika vile inavyotakiwa kitaalamu.

"Kuna mabadiliko makubwa sana kwenye kikosi changu, unaweza kuona sasa baadhi ya wachezaji wameanza kuelewana na wenzao, wanaweza kupiga pasi ambazo wanajua wenzao wanaweza kuzifikia, kila mchezaji ana aina yake ya kupigiwa pasi, mikimbio, kutafuta nafasi, hilo wachezaji wangu wengi walikuwa hawajajuana, lakini kila wanapocheza kuna kitu kipya wanakuja nacho.

Unaweza kuona sasa kila mtu ana spidi, hata wale ambao wamekuwa hawapati nafasi sasa wako fiti na utimamu wa mwili ambapo mwanzo walikuwa wanavikosa, mfululizo wa michezo umesababisha nibadilishe baadhi ya wachezaji ambapo imekuwa na faida sana kwetu, tayari nimeona tuna kikosi kipana cha wachezaji wanaoweza kucheza uwanja kama wale ambao wapo nje, hili limeonekana katika mchezo wetu uliopita dhidi ya Namungo," alisema kocha huyo.

Fadlu alibainisha mpaka ikifika muda ambao unatakiwa, Simba itakuwa moto wa kuotea mbali na kuwa tayari kucheza na timu yoyote ile Afrika, akiwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kufurahi yale maneno kuwa timu bado inajengwa hayatokuwapo tena.

Simba ambayo ina idadi kubwa ya wachezaji wapya wali-

INAENDELEA UKURASA 23

# Mwamnyeto, Job wafichua siri ya ukuta 'jiwe' Yanga

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema wao kama mabeki huwahimiza mastraika wafunge bao moja tu kwani upande wa safu ya ulinzi wana uwezo mkubwa wa kutoruhusu bao kutokana na maelewano makubwa baina yao.

Mchezaji huyo amefichua siri hiyo wakati Yanga ikiwa haijaruhusu bao lolote mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ikicheza michezo saba, ikishinda yote, ikipachika mabao 12, ikikamata nafasi ya pili.

Alisema kwa sasa wapo vizuri sana kwenye kuzuia, hivyo wanapoingia uwanjani huwahimiza mastraika kufunga mabao, na ikiwezekana hata bao moja tu linakuwa tayari limeshawapa pointi tatu.

"Sisi Yanga tukishapata bao moja tu, basi mabeki kazi yetu ni kuzuia bao lisiingie, huwa tunawaambia mastraika wetu wakipata nafasi wazitumie, na ikikosekana hata moja tu, kwa sababu tuna ulinzi imara, ndiyo maana unaona hata likipatikana bao moja halirudi.

"Mpango wetu kwanza huwa ni kupata bao, likishapatikana mengine ni ziada kwa sababu hilo tu linatufanya tuzuie vizuri na tunapata pointi tatu, tunashukuru kwa kucheza kwa maelewano kule nyuma, tumecheza muda mrefu, hivyo kila mmoja anaelewa mwenzake anafanya nini, amekosea wapi na amsaidie vipi," alisema.

Mbali na Mwamnyeto, Yanga ina mabeki wengine kama Ibrahim Hamad 'Bacca', Dickson Job, Yao Kouassi, Shadrack Boka, Nicson Kibabage, na wengine ambao wameifanya safu ya ulinzi kuwa ngumu kupitika msimu huu.

Akizungumzia mchezo wa kesho dhidi ya Singida Black Stars utakaopigwa Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar saa 2:30 usiku, alisema utakuwa ni

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >